# TAASISI
# YA
# ELIMU YA WATU WAZIMA
# TANZANIA

## TAARIFA YA MIAKA 50 YA UHURU (1961 – 2011)

## NA MATARAJIO YA MIAKA 50 IJAYO

Miaka 50

# TAASISI
# YA
# ELIMU YA WATU WAZIMA
# TANZANIA

## TAARIFA YA MIAKA 50 YA UHURU (1961 – 2011)

## NA MATARAJIO YA MIAKA 50 IJAYO

E. Samba
June, 2012

## DIBAJI

Kitabu hiki ni mwitikio wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ambaye aliagiza kila Wizara na Taasisi zake kuandika taarifa ya utekelezaji wa majukumu yake, mafanikio na changamoto katika miaka 50 iliyopita na matarajio ya miaka 50 ijayo. Ni dhahiri kuwa, Mheshimiwa Rais ametoa changamoto kubwa sana katika uwekaji wa kumbukumbu za kihistoria ya taifa la Tanzania kwa miaka mingi ijayo.

Miaka 50 ya uwepo wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) Tanzania, inatoa taswira ya aina yake kwa vile ni chombo pekee kilichokuwa kinatoa na kinaendelea kutoa mchango mkubwa katika kusaidia juhudi za serikali za kuelimisha jamii, ili kuiwezesha kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya nchi.

Nchi yetu ilipopata Uhuru, mwaka 1961, wananchi wengi walikuwa hawana elimu kutokana na mfumo wa elimu wa kikoloni ambao ulilenga kuelimisha watu wachache kukidhi mahitaji ya utawala wao. Kutokana na hili TEWW iliundwa kwa minajili ya kuwaelimisha wananchi waliokosa elimu na waliotaka kujiendeleza kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwemo; kampeni za kitaifa, Redio, machapisho, nyimbo, ngoma, mihadhara, sinema, maigizo, semina, warsha na masomo ya jioni.

Kadiri shughuli za TEWW zilivyokuwa zikiongezeka, ndivyo mchango wake ulivyokuwa unaonekana katika maendeleo ya taifa kwa kuhamasisha na kuelimisha jamii kama inavyofafanuliwa katika kitabu hiki.

Mafanikio ya TEWW katika miaka 50 iliyopita ni pamoja na: kupunguza idadi ya wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu nchini hadi asilimia 9.4 miaka ya 1970 mpaka 1980; kuzawadiwa nishani na shirika la Kimataifa la UNESCO kwa kufanikisha kampeni ya kufuta ujinga Tanzania; kuanzishwa kwa Idara ya Elimu kwa Njia ya Posta

ambayo imewezesha kuelimisha watu wengi mahali waliko kwa njia ya maandishi na vikundi vya majadiliano kupitia redio; kuendesha kampeni za kuelimisha jamii kuhusu masuala mbali mbali ya maendeleo; na kupanua programu za Elimu ya Watu Wazima zinazotoa elimu kuanzia walimu wa kisomo na waendeshaji wa EWW kutoka ngazi ya Astashahada na Stashahada hadi Shahada tangu mwaka 2009.

Kitabu hiki kina kumbukumbu muhimu katika kuboresha mipango ya TEWW ya baadaye kulingana na mahitaji ya taifa kwa ujumla. Pia ni kifungua macho kwa wale ambao walikuwa hawaujui mchango wa Elimu ya Watu Wazima katika mfumo usio rasmi katika kuinua maisha ya watanzania na maendeleo ya nchi. Pia kitabu hiki ni kumbukumbu muhimu kwa vizazi vijavyo.

Mafanikio mengi yaliyojitokeza katika kipindi hicho cha miaka 50 ya uwepo kwa TEWW, yameambatana na changamoto nyingi ambazo zimeathiri utekelezaji wa kazi za Taasisi, zikiwemo: kutokuwa na wataalam wa kutosha waliobobea katika elimu ya watu wazima na mfumo usio rasmi; kutopata ruzuku ya kutosha; na kukosekana kwa miundo mbinu bora na toshelezi. Hata hivyo, TEWW imejipanga kukabiliana na changamoto hizi ili kuboresha mipango ya baadaye ili kuwa na tija na mchango mkubwa katika maendeleo ya sekta ya elimu ya nchi yetu.

Matarajio ya TEWW kwa kipindi cha miaka 50 ijayo ni kupanua mipango yake ikilenga kuchangia maendeleo ya Taifa kwa nguvu zaidi. Kwa mfano TEWW inatarajia: kuanzisha na kuimarisha matawi ya programu katika mikoa ili kuwa na uwezo wa kutoa elimu kwa walengwa wengi zaidi, hasa, katika ngazi za Astashahada, Stashahada na Shahada; kupanua Idara ya Elimu kwa Njia ya Posta kuwa Chuo cha Elimu Masafa (College of Open and Distance Learning) kama linavyohimiza Agizo la Elimu na Mafunzo (Protocal on Education and Training) la Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa

Afrika (Southern Africa Development Community -SADC), sura ya 9 kifungu 4A; kupanua utoaji wa elimu kwa umma katika masuala ya maendeleo kwa kutumia mbinu mbalimbali zinazoendana na wakati kama vile Studio ya kisasa, Maktaba, TEHAMA na machapisho; pia kupanua na kuimarisha miundo mbinu makao makuu na mikoani hasa madarasa, ofisi na kumbi za mikutano, pamoja na usafiri. Lengo ni kuifanya TEWW iwe kituo chenye ubora wa hali ya juu katika kutoa elimu na mafunzo chini ya mfumo usio rasmi, na kuimarisha stadi za kujifunza na jamii yenye uelewa mkubwa wa mambo na kufanya maamuzi sahihi.

TEWW **"Tumethubutu, Tumeweza na Tunasonga Mbele"**

Lambertha H. Mahai
MKURUGENZI

# SHUKRANI


Kitabu hiki kinatoa maelezo ya utekelezaji, mafanikio na changamoto katika shughuli za Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika miaka 50 iliyopita na matarajio ya miaka 50 ijayo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, anatoa shukrani za dhati kwa wale wote ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia katika kukamilisha uandishi wa kitabu hiki.

Kazi hii isingekamilika kama sio jitihada za pekee za kikosi kazi kilichoandika kitabu hiki. Waandishi hawa ni:

Reda Lyimo (Mratibu) ,

Consolata Mongella,

Stanslaus Ntibara,

Placid Balige,

Mugabe Mtani.

Mhariri:

Eric Samba,

Wachangiaji katika Uhariri:

Edward Lugakingira,

Dkt. Wilberforce E. Meena

Mary M. Watugulu,

Mariam B. Kakili,

Bellingtone E. Mariki,

Wachapaji:

Leticia Kulekana,

Zena Rajabu Kazala,

Msaidizi:

Said Mapande.

Mwisho, tunawashukuru pia wengine wote wakiwemo wakuu wa idara na maafisa mbalimbali ambao walitoa michango yao na maoni ya kuboresha toleo la kitabu hiki.

Dkt. Fidelis M. Mafumiko
NAIBU MKURUGENZI
TAALUMA , UTAFITI NA USHAURI

# YALIYOMO

Uk

Dibaji....ii

Shukrani....v

Vifupisho....ix

**1.0 SURA YA KWANZA: USULI....1**

**1.0 Elimu ya Watu Wazima Kabla ya Uhuru....1**

**1.2 Elimu ya Watu Wazima Baada ya Uhuru....3**

**1.3 Kuanzishwa kwa TEWW....5**

**2.0 SURA YA PILI: MUUNDO NA MAJUKUMU YA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA....7**

**2.1 Muundo wa Taasisi ya Watu Wazima....7**

**2.2 Majukumu ya TEWW....9**

**2.3 Historia ya Uongozi wa TEWW....11**

**3.0 SURA YA TATU: UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA KATIKA MIAKA 50 ILIYOPITA....12**

**3.1 Elimu kwa Umma....12**

3.1.1 Kampeni za kuelimisha Jamii....13

3.1.2 Miradi ya Ujasiriamali....14

3.1.3 Tafiti Kuhusu Elimu ya Watu Wazima....16

3.1.4 Machapisho ya Kuelimisha Umma....16

3.1.5 Vikundi vya Mafunzo....18

3.1.6 Mafunzo kwa Redio....19

3.1.7 Harakati za Kudhibiti UKIMWI....20

**3.2 Programu za EWW na Mafunzo Endelezi....21**

3.2.1 Upanuzi wa Programu za Mafunzo....25

3.2.2 Mitaala inayozingatia Umahiri wa Soko la Ajira....27

3.3 Idara ya Elimu kwa Njia ya Posta/ Elimu Masafa..........28

3.3.1 Programu za ENP katika miaka ya 70..........29

3.3.2 Elimu Masafa..........29

3.3.3 Kufanya Utafiti wa Awali..........33

3.3.4 Kuandaa Mitaala..........33

3.3.5 Kuandaa Mihutasari..........33

3.3.6 Utoaji wa Mafunzo Maalum..........34

3.3.7 Moduli Zilizoandikwa..........34

3.3.8 Kuandaa Miongozo..........34

3.3.9 Kuandaa na Kuendesha Mafunzo kwa Waratibu na Walimu wa Vituo vya Elimu Masafa..........34

3.3.10 Uhamasishaji wa Viongozi na Watendaji ngazi ya mkoa na Wilaya..........35

3.3.11 Maandalizi ya Sera ya Elimu Masafa..........35

3.3.12 Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi..........35

**3.4 Uratibu wa Vituo Mikoani..........37**

3.4.1 Shughuli Mbalimbali Ambazo Zinafanya Mikoani..........38

3.5 Utumishi, Utawala na Fedha..........40

**4.0 SURA YA NNE: MAFANIKIO YA TEWW KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 ILIYOPITA..........42**

**5.0 SURA YA TANO: CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI TEWW MIAKA 50 ILIYOPITA..........46**

**6.0 SURA YA SITA: MATARAJIO YA TEWW KATIKA MIAKA 50 IJAYO..47**

**7.0 SURA YA SABA: HITIMISHO..........50**

# VIFUPISHO

1. CBET: Competence Based Education and Training
2. CCP: Chuo Cha Polisi
3. COBET: Complementary Basic Education in Tanzania
4. COL: Common Wealth of Learning
5. DVV: German Adult Education Association
6. ENP: Elimu kwa Njia ya Posta
7. IPPE: Integrated Post Primary Education
8. JAET: Journal of Adult Education
9. MMES: Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari
10. NACTE: National Council for Technical Education
11. ODL: Open and Distance Learning
12. SADC: Southern Africa Development Community
13. SAED: Studies in Adult Education
14. TACAIDS: Tanzania Commission for AIDS Prevention
15. TEHAMA: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
16. TEWW: Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
17. UKIMWI: Upungufu wa Kinga Mwilini
18. UNESCO: United Nations Education, Scientific and Cultural Organization
19. UPE: Universal Primary Education
20. VVU: Virusi Vya UKIMWI

# SURA YA KWANZA

## 1.0 USULI

Tunapoadhimisha miaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara ni vyema tukatafakari na kutathmini jinsi ambavyo "Tumethubutu, Tumeweza na tunavyopaswa Kusonga Mbele" katika sekta ya Elimu, hususan elimu ya watu wazima. Hili linakwenda sambamba na kuangalia jinsi ambavyo Taasisi ya Elimu wa Watu Wazima (TEWW) imeshiriki katika maendeleo ya sekta hii muhimu tangu kupata uhuru. Sura zilizomo katika kitabu hiki zinalenga kueleza historia ya TEWW katika kipindi chote cha miaka 50 ya uhuru wa Tanzania Bara pamoja na muundo wake. Kitabu kinaonyesha, pia, mafanikio ambayo yamepatikana katika kipindi hicho na changamoto zilizoikabili. Mwisho, kitabu kinaelezea dira na malengo maalumu ya TEWW katika miaka 50 ijayo, mkazo ukiwa katika kuelimisha jamii ili iweze kuboresha maisha na kuleta maendeleo ya nchi kwa ujumla.

## 1.1 Elimu ya Watu Wazima Kabla ya Uhuru


### Maana ya Elimu ya Watu Wazima

Elimu ya watu wazima inamaanisha kujifunza chochote kwa shabaha ya kujiendeleza ili kuwa na uwezo zaidi wa kuyamudu mazingira. Hakika ni kujifunza chochote kwa njia na ngazi yoyote ili kumwezesha "mtu kuyaelewa, kuyageuza na kuyatumia mazingira yake ili kuinua hali yake ya maisha" (Nyerere, 1970). Hivyo, elimu ya watu wazima hujumuisha shughuli za kielimu kuanzia kusoma, kuandika na kuhesabu pamoja na shughuli nyingine za kujiendeleza katika stadi na maarifa kama vile elimu ya ufundi, taaluma na stadi za maisha.

Elimu ya watu wazima, na elimu kwa ujumla, katika nchi ya Tanzania, inaweza kutazamwa kwa kuanzia enzi za ukoloni, hususan, kati ya mwaka 1891 na 1945. Wakati huo elimu ya watu wazima ilikuwa ikiendeshwa zaidi na wamisionari. Malengo ya elimu ya watu wazima yalikuwa, kwanza ni kueneza dini kwa kuwasaidia waumini kufuta ujinga ili waweze kusoma

bibilia, kuandika na kujua kuhesabu. Lengo la pili lilikuwa la kisiasa, ambalo lililenga kuwafanya watanganyika kuwa raia wema, yaani raia watiifu kwa serikali ya kikoloni ili kufanikisha mipango yake ya kiutawala. Falsafa hii ya elimu ya kikoloni ilipata kuzungumziwa na hayati Baba wa Taifa mara baada ya uhuru, katika kitabu chake kiitwacho "Ujamaa-Essays on Socialism" , Mwalimu Nyerere alibainisha kuwa:

> Elimu iliyokuwa ikitolewa na serikali ya mkoloni katika nchi zile mbili, Unguja na Tanganyika ambazo sasa ni Tanzania ilikuwa na shabaha tofauti. Haikupangwa ili kuwaandaa vijana kulitumikia taifa lao; badala yake ilipangwa kwa kutimiza haja ya kueneza desturi za kikoloni, na kuwafunza watu waitumikie nchi ya kikoloni (Nyerere, 1968:44).



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere

Hivyo ndiyo kusema kwamba, wakati wa ukoloni kulikuwa na mipango ya elimu ya watu wazima iliyoendeshwa na mashirika ya dini, hasa, chini ya utawala wa Wajerumani na ile iliyoendeshwa na serikali ya Waingereza.

Mipango ya elimu hiyo ya kikoloni ilikuwa na dhima ya kutekeleza na kuimarisha utawala wa kikoloni.

## 1.2 Elimu ya Watu Wazima Baada ya Uhuru

Mara baada ya uhuru, Tanganyika, na baadaye Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, ilihitaji mikakati ya muda mfupi na mrefu ili kuleta maendeleo ya watu wake. Pamoja na mambo mengine changamoto kubwa kielimu ilikuwa ni kiwango kikubwa cha wasiojua kusoma na kuandika. Takwimu zilibainisha kuwa takribani asilimia sabini na tano (75%) ya wanaume wote na asilimia themanini na tano (85%) ya wanawake wote hawakuwa wanajua kusoma na kuandika. Hivyo, moja ya mikakati iliyowekwa ni mpango wa maendeleo wa miaka mitano (5), ambao ulitanguliwa na tamko la rais lililohusu elimu ya watu wazima. Mpango wa kwanza wa miaka mitano (1965-1969) wa maendeleo ya kijamii na kiuchumi uliwasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania mwaka 1964. Mwalimu Nyerere alisisitiza kuhusu umuhimu wa elimu ya watu wazima kwa kusema:

> Kwanza, hatuna budi kuwaelimisha watu wazima. Watoto wetu hawatakuwa na faida katika maendeleo yetu katika miaka mitano, kumi, au hata ishirini ijayo.

Mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano uliazimia kuanzishwa na kuimarishwa, pamoja na mambo mengine, vyombo ambavyo madhumuni yake yalikuwa ni kukuza elimu ya watu wazima. Kwa hiyo, Chuo cha Kivukoni na Chuo cha Viongozi wa Elimu ya Watu Wazima chini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam vilianzishwa (TEWW, 1982). Aidha, ulitolewa ufafanuzi wa falsafa, malengo na umuhimu wa elimu ya watu wazima katika shughuli za maendeleo ya Watanzania. Ufafanuzi huo ulitolewa na Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius K. Nyerere mwaka 1969 katika mkesha wa kuamkia mwaka mpya wa 1970 alipolihutubia taifa kwa njia ya redio. Katika hotuba hiyo, Mwalimu alisisitiza malengo matatu muhimu:

i. Kujitoa katika hali duni ya maisha ambayo watanzania wamekuwa wakiishi katika karne nyingi;

ii. Kijifunza jinsi ya kuongeza ubora wa maisha yetu; na

iii. Kuelewa siasa ya taifa letu ya ujamaa na kujitegemea.

Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi ulihitaji sana raia wenye elimu ya kukidhi mahitaji ya maendeleo ya nchi changa. Hivyo, waasisi wa Taifa hili, pamoja na kutoa dira na mwelekeo wa nchi ya Tanzania, walikuwa na jukumu la kuhakikisha wanatafsiri mwelekeo huo katika vitendo. Mwalimu Nyerere alipofafanua utekelezaji wa malengo ya taifa katika kijitabu cha Azimio la Arusha alisema:

> Azimio la Arusha lililokubaliwa na TANU mwezi Februari 1967 limetimiza haja ya kuwako kwa tamko la ujamaa katika malengo ya Kitanzania, na limetupa mwanzo unaotakiwa wa njia ambayo taifa litaifuata kufikia lengo hilo (Nyerere, 1968: viii).

Mwelekeo huo uliobainishwa na Mwalimu Nyerere ulichangia kuwapo kwa siasa ya Ujamaa na Kujitegemea nchini Tanzania.

Akifafanua kuhusu siasa hiyo ya Ujamaa na Kujitegemea, Mwalimu Nyerere alieleza maana ya neno 'Kujitegemea' ambalo kwa hakika linahusiana sana na malengo ya ujumla ya utoaji wa elimu popote duniani. Mwalimu alianza kwa kuhoji:

> Kumbe kujitegemea maana yake niri basi na kutaleta matatizo gani katika siasa yetu ya siku za baadaye? Kwanza kabisa kujitegemea maana yake ni kwamba hatuna budi kujitegemea sisi na amali zetu wenyewe katika kuleta maendeleo. Amali hizo ni ardhi na watu.

Hivyo basi, kwa kuzingatia siasa na falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea, Tanzania ilielekeza elimu yake kuwa ya Kujitegemea katika mwelekeo huo. Maana yake ni kuwa elimu ilipaswa kumfanya Mtanzania kujikomboa ki-

fikra na kwa kutumia rasilimali zilizopo kujiletea maendeleo yake mwenyewe na kwa jamii inayomzunguka.

Mtazamo huu wa kielimu ulienda sawia na maamuzi ya mkutano mkuu wa UNESCO wa mwaka 1962 ulioliomba Baraza la Umoja wa Mataifa kufikiria mipango ya dharura ya kufanikisha elimu kwa wote ambayo ingeenda sambamba na mpango wa kufuta ujinga kwa watu wazima ifikapo mwaka 2015, ikiwa ni pamoja na kufundisha mambo yote muhimu katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Hivyo malengo haya matatu yalikuwa sababu mojawapo ya uanzishwaji wa chombo maalumu cha kushughulikia elimu ya watu wazima.

## 1.3 Kuanzishwa kwa TEWW

TEWW ni miongoni mwa taasisi za serikali ambazo ziko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi zinazotekeleza sera ya Elimu nchini. Taasisi hii ilianzishwa mwaka 1960, ikiwa ni Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Afrika Mashariki cha Makarere Uganda, chini ya Chuo Kikuu cha London. Kitengo hiki kilikuwa kinatoa elimu ya kujiendeleza kwa watu wazima, hasa wafanyakazi ambao walitaka kujiunga na vyuo vya elimu ya juu. Mwaka 1963, kitengo hiki kilihamishiwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam k ikiwa Kitengo cha Elimu ya Watu Wazima chini ya Idara ya Elimu kwa malengo yale yale. Tangu kuanzishwa kwake, mwaka 1960, shughuli za kitengo ziliendeshwa katika jengo la SUKITA, Mtaa wa Lumumba. Mwaka 1975 kitengo hicho kilifanywa kuwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa sheria ya Bunge Namba 12. Taasisi iliendelea kuwa katika jengo la Mtaa wa Lumumba hadi mwishoni mwa 1992 makao yake makuu yalipohamia Mtaa wa Bibi Titi Mohamed. Majengo yote mawili yanaonekana katika picha namba 1 (a) na (b).



(a) Jengo la Mtaa wa Lumumba ambako TEWW ilianzia kama Kitengo mpaka kuwa Shirika la Umma



(b) Jengo la Mtaa wa Bibi Titi Mohamed ambako makao makuu ya TEWW yalihamia tangu mwaka 1992

Jukumu kuu la TEWW, kama ilivyofafanuliwa katika sheria hiyo ni kutoa elimu ya kujiendeleza na mafunzo ya elimu ya watu wazima kupitia mfumo usio rasmi pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalamu kwa wawezeshaji na wasimamizi wa elimu ya watu wazima.

Taasisi hii ilisajiliwa rasmi na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (National Council for Technical Education - NACTE) mwaka 2005 na kupata ithibati kamili mwaka 2009 ya kutoa mafunzo kwa walimu na waendeshaji wa elimu ya watu wazima katika ngazi za Astashahada (Cheti), Stashahada na Shahada. TEWW inatoa pia elimu ya sekondari kwa vijana nje ya shule, wafanyakazi na watu wazima ambao wanajiendeleza kupitia mfumo wa elimu usio rasmi kwa kutumia njia ya Elimu Masafa na Ana kwa Ana.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inatekeleza majukumu yake kupitia idara sita, nne za taaluma na mbili za utawala, kama inavyofafanuliwa katika sura inayofuata.

# SURA YA PILI

## 2.0 MUUNDO NA MAJUKUMU YA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

Sura hii inaeleza majukumu ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kama yalivyoainishwa katika sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1975. Utekelezaji wa majukumu hayo, unaongozwa na Dira, Dhima na muundo maalumu wa TEWW. Muundo huo utazungumziwa kwa kirefu katika sehemu ya pili ya sura hii. Vilevile, majukumu hayo yanatekelezwa kufuatana na sera za kitaifa.

### Dira ya Teww

Ili kuongeza ubora wa utekelezaji wa majukumu yake, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inaongozwa na dira ifuatayo:

*Kuwa kituo cha Elimu ya Watu W azima na kujiendeleza, chenye ubora wa hali ya juu kinacho sisitiza ujenzi wa jamii iliyoelimika na yenye uelewa mpana na endelevu katika masuala ya kijamii, kitekinolojia, kisiasa na kiuchumi.*

### Dhima

*Kutekeleza sera ya elimu ya watu wazima kwa kubuni, kuandaa, kuratibu na kuendesha programu za mafunzo ya nayowezesha watu wazima kupata maarifa na ujuzi unaohitajika kwa maendeleo endelevu na kuwawezesha walengwa kukabiliana na changamoto za dunia ya wakati uliopo.*


## 2.1 Muundo wa TEWW

Kufuatana na sheria ya Bunge, Namba 12 ya mwaka 1975, iliyoianzisha TEWW, muundo wa Taasisi hii, una Baraza ambalo linaongozwa na Mwenyekiti ambaye huteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu lake kuu ni kusimamia utekelezaji wa majukumu ya TEWW. Mkurugenzi wa TEWW ni Katibu wa Baraza na Mtendaji Mkuu, ambaye husaidiwa na Naibu Wakurugenzi wawili ambao ni: Naibu Mkurugenzi Taaluma, Utafiti na Ushauri na Naibu Mkurugenzi Mipango, Fedha na Utawala.

za Naibu Mkurugenzi Taaluma, Utafiti na Ushauri ni kuratibu na simamia shughuli za idara nne za taaluma ambazo huongozwa na wakuu idara. Idara hizo ni: Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi; Elimu asafa; Elimu kwa Umma na Maendeleo ya Wanawake; na Uratibu wa Vituo koani. Vilevile, anasimamia vitengo vifuatavyo: Utafiti, Mipango, chapisho na Ushauri wa Kitaalam; Mafunzo ya Muda Mfupi; Ushauri asaha na Mitihani.

za Naibu Mkurugenzi Mipango, Fedha na Utawala ni kusimamia endaji katika Idara mbili za uendeshaji ambazo ni Utumishi na Uhasibu, moja na vitengo vya Uchapaji; na Ununuzi. Kielelezo hapa chini naonyesha muundo wa TEWW.

## MUUNDO WA TEWW



## 2.2 Majukumu ya TEWW Kuanzia 1960 Mpaka 1974

Tangu mwaka 1960 mpaka 1974, TEWW ilipokuwa kitengo cha Elimu ya Watu Wazima, ilikuwa na majukumu makuu mawili. Kutoa elimu ya kujiendeleza na kuwapatia mafunzo walengwa waliokuwa wanajiandaa kujiunga na vyuo vya juu. Baada ya mwaka 1969, huduma za TEWW zilipanuka na kuanza kutoa mafunzo ya Stashahada kwa wataalamu wa Elimu ya Watu Wazima, kufanya tafiti na kutoa masomo ya Elimu kwa Njia ya Posta pamoja na Elimu kwa Umma.

## 2.3 Majukumu ya TEWW Kuanzia Mwaka 1975

Kuanzia mwaka 1975, majukumu makuu ya TEWW kufuatana na Sheria ya Bunge Na. 12 ya mwaka 1975 iliyoanzisha Taasisi hii yalipanuliwa, baadhi yake kama ifuatavyo:

a. Kutoa mafunzo ya Astashahada, Stashahada, Stashahada ya Juu na Shahada kwa wataalamu na waendeshaji wa Elimu ya Watu Wazima na huduma za jamii;

b. Kutoa Elimu na mafunzo kwa njia ya masafa kwa vijana nje ya shule, wafanyakazi na watu wazima ambao wanajiendeleza katika mfumo wa elimu usio rasmi;

c. Kufanya tafiti na tathmini za EWW na kutoa matokeo kwa jamii;

d. Kuishauri Serikali, taasisi nyingine zinazotoa huduma za kijamii pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu uandaaji wa mitaala na mbinu za kufundisha watu wazima;

e. Kubuni, kuratibu na kuendesha kampeni mbalimbali za kitaifa kwa kushirikiana na serikali, taasisi na mashirika mengine kuhusu kisomo, kilimo bora, afya, demokrasia, mazingira, utawala bora, UKIMWI na masuala mengine mtambuka;.

f. Kutoa mafunzo ya Cheti cha Sheria kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam;

g. Kuandaa na kushiriki katika mikutano, midahalo, warsha na semina zinazohusiana na shughuli za taasisi ndani na nje ya nchi; na

h. Kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu elimu ya watu wazima na elimu ya mfumo usio rasmi kwa serikali, mashirika, taasisi na jamii kwa ujumla.

## 2.4 Historia ya Uongozi wa TEWW

Tangu ilipoanzishwa hadi sasa TEWW imeongozwa na viongozi wakuu tisa. Kati ya hao tisa, watatu walitoka nje ya Tanzania. Aidha kati ya hao viongozi tisa, wawili ni wanawake.

Zifuatazo ni picha za viongozi wa TEWW tangu mwaka 1963 hadi 2012.




*1963 – 1967: Paul Bertulsen*




*1967 – 1970: Dorothy Thomas*




*1970 – 1973: Paul Mhaiki*




1973 – 1979: Fr. Dk. Daniel Mbunda



1979 – 1981: Yusuph Kassam



1981 – 1982: Pius Ng "wandu



1982 – 1991: Esperius Ntirukigwa



1991 – 2003: Jumanne Mayoka



2004 – sasa: Lambertha Mahai

# SURA YA TATU

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA KATIKA MIAKA 50 ILIYOPITA

Sura ya kwanza imefafanua kuhusu shughuli za Elimu ya Watu Wazima zilivyokuwa zinaendeshwa kabla ya Uhuru hadi kufikia mwaka 1975 ambapo TEWW iliundwa rasmi kama shirika la umma chini ya Wizara ya Elimu ya Taifa wakati huo. Sheria iliyoiunda Taasisi hii inafafanua muundo na majukumu yake. Baraza la TEWW husimamia utekelezaji wa majukumu yote likiongozwa na Mwenyekiti. Mtendaji mkuu wa shughuli za kila siku za TEWW ni Mkurugenzi ambaye husaidiwa na Naibu Mkurugenzi Taaluma, Utafiti na Ushauri; na Naibu Mkurugenzi Mipango, Fedha na Utawala. Majukumu makuu ya TEWW yanafafanuliwa katika maeneo kadhaa.

### 3.1 Elimu kwa Umma

Lengo kuu la kuanzisha Elimu kwa Umma lilikuwa kutoa mafunzo ya kujiendeleza hasa kwa wale waliotaka kujiunga na elimu ya juu. Hivyo, TEWW ilijikita zaidi katika kuandaa, kuendesha na kuratibu masomo ya jioni, semina za kila wiki na mafunzo mengine ambayo yalilenga kuwaandaa watu wazima waliotaka kujiunga na chuo kikuu.

Baada ya uhuru, serikali iliona umuhimu wa kupanua na kuimarisha elimu ya watu wazima ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya nchi yao. Tangu wakati huo shughuli za kuelimisha umma ziliendelea kupanuka ili kuwafikia wananchi wengi waweze kupambana na changamoto katika kuboresha maisha yao ya kila siku. Mbinu mbalimbali zilitumika kufikisha ujumbe kwa walengwa kwa kuzingatia zaidi kuwa watu wazima hujifunza kwa kuona, kutenda na kushiriki.

Ili kwenda sambamba na upanuzi huo, TEWW ilibuni na kutumia mbinu mbalimbali za kuelimisha umma. Mbinu hizo zilijumuisha:

### 3.1.1 Kampeni za kuelimisha Jamii

Taasisi iliandaa, kuratibu na kuendesha kampeni za kitaifa za kuelimisha umma kuhusu masuala mtambuka ya maendeleo zikiwemo:

a) **Uchaguzi ni Wako** (1968), ambayo iliendeshwa kitaifa ili kuhamasisha na kuelimisha jamii namna ya kupiga kura katika uchaguzi wa kwanza baada ya uhuru.

b) **Kupanga ni Kuchagua** (1968), iliyoendeshwa kwa ajili ya kushirikisha wananchi katika mpango wa kwanza wa maendeleo wa miaka mitano.

c) **Kisomo cha Watu Wazima** (1970), iliyoendeshwa ili kufuta ujinga wa kutokujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

d) **Wakati wa Furaha** (1971), iliyolenga kupima maendeleo ya wananchi baada ya miaka kumi ya Uhuru.

e) **Siasa ni Kilimo** (1973), iliyolenga kudumisha kilimo cha kisasa ili kuleta maendeleo.

f) **Mtu ni Afya** (1974), iliyoelimisha jamii kuhusu namna ya kujikinga na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuhara damu na mengine. Ilisisitiza umuhimu wa kuwa na mazingira mazuri ya kuishi.

g) **Chakula ni Uhai** (1975), iliyoelimisha jamii kuhusu mambo makuu mawili:

i) Uzalishaji mazao ya chakula; na

ii) Uandaaji na umuhimu wa lishe bora.

h) **Misitu ni Mali** (1980), ambayo ililenga kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kutunza misitu ili kuzuia kuenea kwa jangwa Tanzania.

i) **Elimu kwa Wapiga Kura** (1995), iliyolenga kuelimisha jamii kuhusu demokrasia na namna ya kushiriki kugombea na kupiga kura katika uchaguzi wa mfumo wa vyama vingi vya siasa.

j) **Tubadili Tabia Tuushinde UKIMWI** (2001), kampeni ya kitaifa dhidi ya janga la UKIMWI iliyoendeshwa kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti

UKIMWI Tanzania (TACAIDS) na kuandaa mpango wa miaka 5 (2000-2005) wa kupambana na janga hilo. Mpango huu ulijumuisha watoto wa shule, vijana na watu wazima na ulilenga kuwa na taifa lisilo na UKIMWI ifikapo 2015.

k) **Mafunzo ya Sheria ya Gharama za Uchaguzi** (2010), ambayo ilielimisha wananchi kuhusu sheria mpya ya gharama za uchaguzi ili waielewe na kushiriki waweze kushiriki katika kutekeleza yaliyofafanuliwa katika sheria hiyo.



Uzinduzi wa kampeni ya kuelimisha umma kuhusu sheria ya gharama za uchaguzi

### 3.1.2 Miradi ya Ujasiliamali

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, kupitia Idara ya Elimu kwa Umma, ilianzisha seksheni ya Maendeleo ya Wanawake mwaka 1974. Katika harakati za kuwawezesha wanawake kujikomboa kielimu na maendeleo ya maisha yao, seksheni hiyo ilijikita zaidi katika kuhamasisha na kusaidia, kuanzisha na kuratibu miradi mbalimbali ya kiuchumi kwa vikundi vya wanawake. Katika vikundi hivyo, wanawake walipata elimu pamoja na kuongeza pato lao lililoboresha maisha yao na ya familia zao kwa ujumla.

Taasisi iliweza kuanzisha miradi kwa kushirikiana na vikundi hivyo. Baadhi ya miradi hiyo ni kama ilivyoorodheshwa katika jedwali namba I.

**Jedwali Na I: Miradi ya Vikundi vya Wanawake**

| Mwaka | Jina la Kikundi | Aina ya Mradi | Mkoa Ulipo Mradi |
|---|---|---|---|
| 1975 | Chiwanda | Elimu ya Lishe | Ruvuma |
| 1977 | Mawella | Elimu ya Ushonaji | Kilimanjaro |
| 1977 | Msindo | Elimu ya Lishe Bora | Ruvuma |
| 1978 | Kyagata | Mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ng'ombe wa maziwa | Mara |
| 1978 | Pugu Kajiungeni Mradi wa Ufugaji kuku | Mafunzo kuhusu Lishe Bora | Dar es Salaam |
| 1979 | Kikundi cha kina mama Geita | Lishe Bora | Mwanza |
| 1979 | Chala Nkasi | Mafunzo kuhusu ufugaji bora wa ng "ombe wa maziwa | Rukwa |
| 1979 | Kikundi cha majengo Arusha | Mafunzo kuhusu mbinu za kuanzisha na kuendesha maduka ya ushirika | Arusha |
| 1980 | Vikundi cha wanawake vya maduka | Mafunzo ya Ujasiliamali | Arusha |

Seksheni hiyo, pia, ilikuwa inaendesha mafunzo ya ushonaji kwa wasichana ambao walitaka kujiendeleza katika ushonaji. Walengwa walikuwa wanajifunza kwa vitendo kwa hiyo walipata elimu na maarifa ya kuendesha miradi na kupata pato lililosaidia kuboresha maisha yao ya kila siku. Pia, inafanya tafiti mbalimbali na kuandika vitabu vya "Sauti ya Wanawake" kutokana na matokeo ya utafiti huo.



Wanafunzi wa ushonaji wakielekezwa na mwalimu wao darasani, TEWW makao makuu

### 3.1.3 Tafiti Kuhusu Elimu ya Watu Wazima

Kabla ya kupanga mpango wowote wa kuelimisha jamii ni lazima kufanya utafiti wa awali. Kwa hiyo, TEWW iliendesha tafiti mbalimbali kuhusu elimu ya watu wazima katika masuala mtambuka ya maendeleo. Tafiti hizo zilitumika kuandaa machapisho ya kuelimisha umma, kama vile jarida la Elimu ya Watu Wazima liitwalo "Journal of Adult Education in Tanzania (JAET)", matoleo 18; Jarida la Tafiti katika Elimu ya Watu Wazima liitwalo "Studies in Adult Education (SAED)", matoleo 16; na Jarida la Wanawake liitwalo "SAUTI YA WANAWAKE" matoleo matano.

### 3.1.4 Machapisho ya Kuelimisha Umma

Machapisho ni mbinu mojawapo ya kuelimisha watu popote pale walipo. TEWW iliandaa na kuchapa vitabu, majarida na vipeperushi mbalimbali vya kuelimisha umma katika masuala ya maendeleo. Machapisho hayo ni kama yalivyooneshwa katika jedwali namba 2.

**Jedwali Na 2: Baadhi ya Machapisho ya TEWW**

| Na. | Jina la Kitabu/Jarida | Mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Elimu ya Mradi wa Kiuchumi | 1996 |
| 2. | Usawa na Maisha Bora ya Familia | 1996 |
| 3. | Jifunze kusoma, kuandika na kuhesabu | 1996 |
| 4 | Endeleza familia yako | 1996 |
| 5. | Maisha Marefu katika Nyumba Bora – Mkoa wa Singida | 1992 |
| 6 | Madhara ya Kutahili/Kukeketa Wanawake | 1992 |
| 7 | Kilimo cha Kisasa Mkoani – RUKWA | 1991 |
| 8 | Kilimo cha Ufugaji Bora – PWANI | 1991 |
| 9 | Kuimarisha Afya Bora – PWANI | 1991 |
| 10 | Tuwe na Afya Bora Mkoani – RUVUMA | 1991 |
| 11 | Hifadhi Mazingira – TABORA | 1991 |
| 12 | Ongezeko la Watu | 1991 |
| 13 | Matunzo ya Mama Mjamzito | 1991 |
| 14 | Kilimo cha Maksai – RUVUMA | 1990 |
| 15 | Tudumishe Afya Bora – TANGA | 1990 |
| 16 | Tutatue Matatizo yetu Wenyewe Mwanzo Mgumu | 1990 |
| 17 | Zijue Haki za Mtoto | 1990 |
| 18 | Magonjwa Hatari kwa Mtoto | 1990 |
| 19 | Tutatue Matatizo Wenyewe: mwanzo mgumu | 1990 |
| 20 | Mbinu za Kilimo na Ufugaji Bora Mkoani Rukwa | 1990 |
| 21 | Afya Mkoani – MARA | 1989 |
| 22 | Uvuvi Mkoani – RUVUMA | 1989 |
| 23 | Uvuvi Mkoani – MARA | 1989 |
| 24 | Yajue Magonjwa 10 ya Hatari kwa Watoto | 1989 |
| 25 | Afya Bora Mkoani – MWANZA | 1988 |
| 26 | Malezi Bora Mtoto | 1988 |
| 27 | Kupambana na Magonjwa ya Hatari mkoani – MBEYA | 1987 |
| 28 | Kuimarisha Kilimo na Mifugo – MBEYA | 1987 |
| 29 | Afya kwa Maendeleo – KIGOMA | 1987 |
| 30 | Mbinu za Kufanikisha Kilimo – KIGOMA | 1987 |
| 31 | Ufugaji na Ukulima wa Kisasa – KIGOMA | 1987 |
| 32 | Jikinge na Magonjwa Hatari – KILIMANJARO | 1987 |
| 33 | Matumizi ya choo bora | 1987 |
| 34 | Kiongozi cha Mradi wa Kukoboa | 1987 |
| 35 | Matumizi ya Choo Bora | 1987 |
| 36 | Jiandae Kupata Mtoto | 1987 |
| 37 | Afya Bora Mkoani – KAGERA | 1986 |
| 38 | Mbinu Bora za Kilimo Mkoani – KAGERA | 1986 |
| 39 | Sauti ya Wanawake Tanzania 1-3 | 1985 |
| 40 | Mbinu za Kilimo Bora cha Mazao | 1985 |
| 41 | Mafanikio ya Kilimo Bora – DODOMA | 1985 |
| 42 | Ufugaji Bora Mkoani – MWANZA | 1985 |

| Na. | Jina la Kitabu/Jarida | Mwaka |
|---|---|---|
| 43 | Mazao ni Uhai wa Taifa – MOROGORO | 1984 |
| 44 | Mifugo ni Uchumi na Shibe | 1984 |
| 45 | Zijue Haki za Watoto Wetu | 1984 |
| 46 | Inua na Imarisha Uchumi Wetu – SHINYANGA | 1983 |
| 47 | Jifunze Kushona Nguo za Watoto | 1983 |
| 48 | Tutatue Matatizo yetu wenyewe – IRINGA | 1982 |
| 49 | Matunda ya Ufugaji Bora – Mkoa wa IRINGA | 1982 |
| 50 | Bepari alieyekubali Ujamaa | 1980 |
| 51 | Tusimuliane Hadithi Zetu | 1980 |
| 52 | Faida ya Ufugaji wa Kuku | 1980 |
| 53 | Bahati ya Mdudu | 1980 |
| 54 | Elimu ya Vikundi vya Mafunzo | 1979 |
| 55 | Uvuvi Bora Tanzania | 1979 |
| 56 | Samaki ni Chakula Bora pia ni Mali | 1979 |
| 57 | Kazi ni Ubinadamu | 1979 |
| 58 | Usiku wa Ngoma | 1971 |
| 59 | Pamba Yamrudia Mkulima | 1971 |
| 60 | Elimu ya Vikundi vya Mafunzo | 1971 |
| 61 | Bustani ya Nyumbani | 1971 |

Mengi ya machapisho haya yaliandikwa kwa msaada wa Chama cha Elimu ya Watu Wazima cha Ujerumani (DVV), kilichofadhili TEWW kwa miaka kumi na miwili; UNICEF, chini ya mradi wa "Mama na Mtoto" miaka ya 1980; na UNESCO, vitabu vyenye mtazamo wa kijinsia katika miaka ya 1990.

### 3.1.5 Vikundi vya Mafunzo

Vikundi ni mojawapo ya mbinu ambazo zilitumika katika kufundisha watu wazima. Mbinu hii hushirikisha wanakikundi katika majadiliano ya mada. Kikundi kimoja kinatakiwa kisizidi idadi ya watu 15 na pawepo na mshauri ambaye atakiongoza kikundi.

Njia ya majadiliano katika vikundi ilitumika ikiongozwa na vipindi vya redio au kanda na vitabu vya mafunzo. Vitabu vilivyotumika viliandikwa katika lugha rahisi ili viweze kusomwa kwa urahisi na wananchi ambao wengi wao ni wanakisomo huko vijijini.

Vikundi vya mafunzo vilikuwa vikiundwa mapema kabla ya mafunzo kuanza. Vikundi hivi vilikuwa vinaongozwa na mlezi, mwenyekiti na mratibu.

### 3.1.6 Mafunzo kwa Redio

Baada ya Uhuru shughuli za kuelimisha umma zilipanuka hivyo ilibidi Idara ya Elimu kwa Umma kutumia mbinu mbalimbali kufikisha ujumbe kwa walengwa wengi huko vijijini.

Pamoja na mbinu nyingine, elimu ilitolewa pia kwa redio na wananchi, katika vikundi vyao, waliweza kujifunza kwa kusikiliza na kujadiliana somo kwa kuongozwa na mwezeshaji wa kikundi.

Wakati wa kuendesha kampeni za kuelimisha umma, mafunzo kwa redio yalitumika sana. Wakati huo kulikuwepo na Studio kubwa moja tu ya Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD), ambayo ilikuwa inarusha matangazo ya kuelimisha umma. Studio nyingine ndogo ndogo pia zilikuwa zinatoa mafunzo kupitia RTD, ambayo ilitenga vipindi maalumu kwa ajili ya EWW.

Katika mwaka 1975, wakati TEWW ilipoundwa rasmi na sheria ya Bunge Na. 12, TEWW ilianzisha studio ndogo ya kuandaa masomo ya watu wazima na kuyarusha kwa walengwa kupitia RTD. TEWW iliweza pia kuandaa sinema za mafunzo zilizoonyeshwa kwa wanavijiji kwa kutumia magari.

Mwaka 1992 mwishoni, Makao Makuu ya TEWW yalihamia jengo la Elimu kwa Njia ya Posta lililoko Mtaa wa Bibi Titi Mohamed kiwanja namba 7, Kisutu, ambako imejenga Studio ya kisasa kwa ajili ya kuandaa mafunzo ya kujiendeleza na kuyarusha kupitia Studio mbalimbali zilizopo nchini Mpango wa baadaye kwa Studio hiyo ya TEWW ni kuiwezesha kurusha Mafunzo ambayo walengwa wataweza kujifunza popote walipo hapa nchini.



Studio Mpya ya TEWW inayotumia Vifaa na Tekinolojia ya Kisasa

### 3.1.7 Harakati za Kudhibiti UKIMWI

Harakati za kudhibiti UKIMWI zimehusisha shughuli zifuatazo:

i) Mwaka 2001, Idara iliandaa kampeni na mpango wa miaka mitano wa kupambana na janga la UKIMWI, wenye kauli mbiu " Badili Tabia Tuushinde UKIMWI". Mpango huu ulitekelezwa kwa kushirikiana na Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI (Tanzania AIDS Control Commission - TACAIDS). Mkakati ulianza kwa kutoa mafunzo ya wawezeshaji kitaifa na kanda; na ulilenga kwenda hadi kijijini na kuwa na mpango wa miaka mitano ya utekelezaji katika ngazi zote. TEWW iliandaa wawezeshaji ngazi za kitaifa, mkoa na wilaya. Wilaya ziliendelea na kuwezesha na kuhamasisha ngazi za kata, vijiji na vitongoji.

ii) Iliandaa pia programu ya mafunzo ya kudhibiti UKIMWI kwa kuhamasisha wanajamii kupima afya zao kwa hiari, wakiwemo wafanyakazi wa TEWW wa makao makuu na mikoani, pamoja na

wanafunzi. Matokeo yake ni kwamba TEWW ilianza kuwek kumbukumbu za wafanyakazi wanaoishi na virusi vya UKIMWI n kuwapatia huduma stahili. Programu hii ilifanywa kuwa ya kitaifa.

iii) Pia, kwa kushirikiana na wataalamu wengine, Taasisi imeanda rasimu ya mpango mkakati wa TEWW wa kudhibiti UKIMWI sehem za kazi.

iv) Mwaka 2007 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ilianzisha kitengo ch Ushauri Nasaha kwa ajili ya kuhudumia wafanyakazi na wanafun wanaoishi na Virusi vya UKIMWI.

v) Vilevile, TEWW iliandaa kitabu cha Mwongozo wa Kutoa Elimu ya UKIMWI Katika Mfumo Usio Rasmi.




Semina ya UKIMWI kwa Wafanyakazi wa TEWW Makao Makuu (2007)

### 3.2 Programu za Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi

Uandaaji wa mitaala, usimamizi na uratibu wa programu zote za Elimu y Watu Wazima na Mafunzo Endelezi zinazotolewa na TEWW zinaanzia nga ya Astashahada hadi Shahada. Msfunzo haya yalianza tangu mwaka 196

TEWW ikiwa kitengo chini ya Idara ya Elimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Kitengo hiki kilianza rasmi kutoa mafunzo ya stashahada ya elimu ya watu wazima mnamo mwaka 1969 baada ya tafiti na tathmini zilizofanywa kuhusu umuhimu wa kuanzisha programu hiyo.

Mafunzo hayo yalilenga kuwanufaisha maafisa wasimamizi na waendeshaji wa programu za elimu ya watu wazima katika kata, wilaya, mkoa na taifa kwa jumla.

Mafunzo haya yaliendelea kutolewa na kitengo hiki mpaka mnamo mwaka 1975, kilipopewa mamlaka ya kuwa taasisi ya umma inayojitegemea, chini ya Wizara ya Elimu, kwa Sheria Namba 12 ya Bunge la Jamhuri ya Muungano ya mwaka huo.

Tangu kuundwa kwake, TEWW imeendelea kuwa taasisi pekee katika Tanzania inayozalisha wataalam wa Elimu ya Watu Wazima katika ngazi ya Stashahada. Wataalam hawa wamekuwa tegemeo kubwa la taifa katika kusimamia, kutekeleza na kutoa ushauri mbalimbali kuhusu masuala ya elimu ya watu wazima hasa katika kata na wilaya. Kati ya mwaka 1990 na 1995, kwa kuzingatia mahitaji na umuhimu wa wataalam wa elimu ya watu wazima, TEWW ilianzisha programu ya Stashahada ya Juu pamoja na Astashahada ili kuweza kukidhi mahitaji ya wataalam wa kuwezesha na kusimamia elimu ya watu wazima katika ngazi zote. Mafunzo ya Astashahada yalitolewa katika kituo cha TEWW cha mafunzo na mikutano, WAMO, kilichopo mkoani Morogoro.



**Baadhi ya Majengo ya Kituo cha Mikutano na Mafunzo, WAMO -Morogoro**

Aidha, mafunzo ya Stashahada yamekuwa yakitolewa kwa washiriki toka Tanzania na nchi nyingine za bara la Afrika kama vile Uganda, Kenya, Ethiopia, Msumbiji, Afrika Kusini, Gambia, Eritrea, Zimbabwe na Somalia. Jedwali namba 3 hapa chini linaonyesha idadi ya wanafunzi walioandikishwa na kupata mafunzo katika programu ya Stashahada kati ya mwaka 1969 hadi 2011.

**Jedwali Na. 3: Wanafunzi waliosajiliwa kwa Ajili ya Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima: 1969 - 2011**

| Mwaka | Jinsi | | Jumla | Kutoka nje ya nchi |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | | |
| 1969/70 | 20 | 3 | 23 | |
| 1970/71 | 23 | 1 | 24 | |
| 1971/72 | 25 | 3 | 28 | |
| 1972/73 | 26 | 2 | 28 | |
| 1973/74 | 26 | 4 | 30 | |
| 1974/75 | 27 | 2 | 29 | |
| 1975/76 | 26 | 9 | 35 | |
| 1976/77 | 33 | 12 | 45 | |
| 1977/78 | 43 | 11 | 54 | |
| 1978/79 | 44 | 11 | 55 | |
| 1979/80 | 46 | 12 | 58 | 2 Gambia |
| 1980/81 | 37 | 7 | 44 | 4 Msumbiji |
| 1981/82 | 40 | 6 | 46 | 1 Uganda, 2 Afrika Kusini, 4 Msumbiji |
| 1982/83 | 28 | 11 | 39 | 1 Zimbabwe |
| 1983/84 | 44 | 12 | 56 | |
| 1984/85 | 31 | 14 | 45 | 1 Uganda |
| 1985/86 | 40 | 11 | 51 | |
| 1986/87 | 39 | 16 | 55 | 1 Uganda |
| 1987/88 | 45 | 12 | 57 | |
| 1988/89 | 37 | 20 | 57 | 1 Uganda |
| 1989/90 | 33 | 7 | 40 | 1 Afrika Kusini, 1 Kenya, 1 Uganda |
| 1990/91 | 30 | 11 | 41 | 2 Kenya, 1 Uganda, 5 Afrika Kusini |
| 1991/92 | 34 | 12 | 44 | 1 Uganda, 3 Kenya, 5 Afrika Kusini |
| 1992/93 | 39 | 6 | 45 | 3 Kenya, 4 Afrika Kusini |
| 1993/94 | 24 | 13 | 37 | 3 Uganda, 4 Kenya |
| 1994/95 | 28 | 16 | 44 | 3 Kenya |
| 1995/96 | 36 | 4 | 40 | 3 Kenya, 2 Uganda, Eritrea |
| 1996/97 | 36 | 22 | 58 | |
| 1997/98 | 30 | 18 | 48 | |
| 1998/99 | 35 | 29 | 64 | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1999/2000 | 20 | 20 | 40 | |
| 2000/2001 | 33 | 28 | 61 | |
| 2001/2002 | 42 | 32 | 74 | |
| 2002/2003 | 43 | 29 | 72 | |
| 2003/2004 | 48 | 39 | 87 | |
| 2004/2005 | 39 | 75 | 114 | |
| 2005/2006 | | | | |
| 2006/2007 | 97 | 61 | 158 | |
| 2007/2008 | 79 | 47 | 126 | |
| 2008/2009 | 100 | 119 | 210 | |
| 2009/2010 | 72 | 80 | 152 | |
| 2010/2011 | 136 | 152 | 288 | |
| JUMLA | 1,694 | 992 | 2,677 | |

**Chanzo: Taarifa za TEWW**

Wahitimu wa mafunzo ya Elimu ya Watu Wazima katika ngazi hizi (Astashahada na Stashahada) hupangiwa na serikali kusimamia shughuli za elimu katika ngazi za kata na wilaya kama vile Waratibu wa Elimu (Kata); Afisa Elimu (Wilaya); Waratibu Elimu ya Watu Wazima (Wilaya); Afisa Vielelezo na Takwimu na Afisa Taaluma na Mkaguzi wa Elimu ya Msingi (Wilaya). Pia wahitimu hao hufundisha madarasa ya Elimu ya Watu Wazima na Shule za sekondari na msingi. Wengine huteuliwa kuwa wakuu wa shule hizo na wamekuwa watendaji wazuri wenye kumudu shughuli za uongozi.



Waziri wa Elimu ya Taifa wakati huo, Nicolas Kuhanga, akionesha cheti cha Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima siku ya mahafali ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima , mnamo tarehe 27 Mei 1978.

### 3.2.1 Upanuzi wa Programu za Mafunzo

Ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira, programu ziliboreshwa na kuwa za mafunzo yanayozingatia zaidi umahiri kwa wahitimu. Maboresho hayo yalitoa fursa pia kwa watendaji wa maendeleo ya jamii kupata elimu kupitia TEWW. Mwaka 2009, programu zilipanuliwa kufikia ngazi ya shahada baada ya serikali kuagiza kufuta Stashahada ya Juu ili kwenda sambamba na mahitaji ya sera za nchi nyingine za Afrika Mashariki na Jumuia ya Kusini mwa Afrika.

Hatua hii ilisababisha kubadilisha mfumo mzima wa utoaji mafunzo ya programu za TEWW kutoka mfumo uliokuwa unazingatia maarifa (Knowledge Based Education and Training - KBET) na kufuata unaozingatia zaidi umahiri wa kazi katika maisha ya kila siku na mahitaji ya soko la ajira yaani Competence Based Education and Training (CBET). Mafunzo haya yamekuwa yakiwanufaisha maafisa wasimamizi na uendeshaji wa programu za Elimu ya Watu Wazima, katika ngazi za kata, wilaya, mkoa na hata taifa.

Majedwali Na. 4 na 5 yanaonesha idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika mafunzo ya ngazi ya Stashahada ya Juu na Shahada tangu mwaka 2005/2006 hadi 2010/2011.

**Jedwali Na. 4: Wanafunzi Walioandikishwa kwa ajili ya Stashahada ya Juu ya Elimu ya Watu Wazima na Maendeleo ya Jamii**


| Mwaka | Jinsi | | Jumla | Kutoka nje ya nchi |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | | |
| 2005/2006 | 46 | 17 | 63 | - |
| 2006/2007 | 74 | 46 | 120 | - |
| 2007/2008 | 70 | 39 | 107 | - |
| 2008/2009 | 57 | 71 | 128 | - |
| JUMLA | 247 | 173 | 418 | - |

**Jedwali Na. 5: Wanafunzi Walioandikishwa kwa ajili ya Shahada ya Elimu ya Watu Wazima**

| Mwaka | Jinsi | | Jumla | Kutoka nje ya nchi |
|---|---|---|---|---|
| | Wanaume | Wanawake | | |
| 2009/2010 | 52 | 59 | 111 | - |
| 2010/2011 | 70 | 57 | 127 | - |
| JUMLA | 122 | 116 | 238 | - |

Wahitimu katika ngazi hizo (Stashahada ya Juu na Shahada) wanapohitimu mafunzo hurudi katika sehemu zao za kazi au hupangiwa na Wizara ya Elimu kusimamia shughuli za elimu katika ngazi za Taifa, Mkoa, Wilaya na Kata, kama vile Afisa Elimu ya Watu Wazima (Mkoa); Afisa Elimu (Wilaya); Waratibu Elimu ya Watu Wazima (wilaya); Afisa Vielelezo na Takwimu, Afisa Taaluma (Wilaya) na wakuu wa shule za msingi. Pia wahitimu hawa hufundisha Shule za sekondari pamoja na kuendeleza shughuli za elimu ya watu wazima na miradi ya maendeleo ya jamii katika mashirika yasiyo ya kiserikali, ambayo yanahitaji kada hii ya wataalam, hasa ngazi ya wilaya na kata.

### 3.3 Elimu kwa Njia ya Posta/Elimu Masafa



Wanafunzi wakiwa Darasani



Mahafali ya TEWW

### 3.2.2 Mitaala inayozingatia Umahiri na Soko la Ajira


Kwa kushirikiana na NACTE pamoja na wadau mbalimbali wa elimu ya watu wazima ilifanya utafiti wa awali uliosaidia kubaini mahitaji na maudhui sahihi ya elimu kwa walengwa. Kufuatana na utafiti huo, mitaala mipya inayozingatia mahitaji ya soko la ajira iliandaliwa na kuchapishwa.



**Wakufunzi wa TEWW Wakiandaa Mitaala ya CBET**

Elimu kwa Njia ya Posta (ENP)/Elimu Masafa inamaanisha utoaji wa elimu kwa mwanafunzi akiwa mbali na mwalimu wake, kwa kutumia njia mbali mbali za mwasiliano. Picha ifuatayo inaonyesha baadhi ya njia hizo.

Njia Mbalimbali za Elimu kwa Njia Masafa na Ana kwa Ana.




ENP ilianzishwa TEWW mwaka 1970 kwa msaada wa International Development Agency (SIDA) ikiwa na lengo la kuwafikia watanzania wengi ambao hawakupata fursa ya kupata elimu kupitia mfumo rasmi. Miongoni mwao ni wafanyakazi, wakulima na wahitimu wa elimu ya msingi. TEWW inafanya kazi kupitia vituo vyake vyote 21 vilivyopo mikoani. Vituo hivi huratibu na kusajili wanafunzi wote wanaojiunga na programu zinazotolewa kwa njia ya elimu masafa na masomo ya ana kwa ana. Pia, hutoa huduma mbalimbali kama vile ushauri kwa walengwa, kusambaza moduli, kutoa mazoezi, mitihani, kusahihisha na kazi nyingine zinazotolewa na walimu. Huduma hizo huwarahisishia wanafunzi kusoma masomo yao kwa ufanisi.

### 3.3.1 Programu za ENP katika Miaka ya 1970

Kati ya mwaka 1972 na 1989, TEWW iliweza kuandaa na kuendesha programu mbalimbali kama vile Elimu kwa umma, Elimu ya sekondari, Mafunzo ya utaalam, Elimu maalum na mafunzo ya walimu tarajali kwa mpango wa Elimu kwa Wote (Universal Primary Education – UPE) na Mafunzo ya walimu kazini mwaka 1974 - 1987. Programu hizi zililenga kuwanufaisha watu mbalimbali kama vile walimu, walemavu na watu wa kawaida wanaojua kusoma na kuandika (wakulima). Mafunzo haya yalitolewa katika vituo vya kata. Waratibu wa tarafa na kata waliopata mafunzo kwa miezi miwili waliweza kuwa wawezeshaji katika vituo hivyo. Idadi yao ilikuwa 2,400. Mafunzo yalianza rasmi mwaka 1976 na kati ya mwaka 1976 na 1986, jumla ya walengwa 57,524 walikuwa wamekwisha jiunga katika programu hizo. Walengwa 15,135 walifanya mafunzo ya ualimu daraja IIIC.

### 3.3.2 Elimu Masafa

Mahitaji ya jamii na maendeleo ya sayansi na teknolojia yamefanya TEWW kurekebisha mfumo wa Elimu kwa Njia ya Posta na Masomo ya Jioni ya Kujiendeleza kuwa mfumo wa Elimu Huria na Masafa. Jedwali namba 6 linaonesha idadi ya wanafunzi waliodahiliwa chini ya mfumo wa awali wa Elimu kwa Njia ya Posta na masomo ya jioni ya kujiendeleza, mwaka 1972 mpaka 2003.

**Jedwali Na 6: Udahili wa Wanafunzi wa Elimu kwa Njia ya Posta na Masomo ya Jioni ya Kujiendeleza**

| Mwaka | Wanaume | Wanawake | Jumla |
|---|---|---|---|
| 1972 | 334 | 40 | 374 |
| 1973 | 4993 | 347 | 5340 |
| 1974 | 5511 | 487 | 5998 |
| 1975 | 5421 | 574 | 5995 |
| 1976 | 5477 | 937 | 5995 |
| 1977 | 5751 | 1291 | 5995 |
| 1978 | 5066 | 1313 | 6379 |
| 1979 | 3009 | 767 | 3776 |
| 1980 | 1647 | 243 | 1890 |
| 1981 | 2534 | 647 | 3181 |
| 1982 | 2741 | 716 | 3457 |
| 1983 | 3042 | 752 | 3794 |
| 1984 | 2580 | 750 | 3330 |
| 1985 | 1401 | 369 | 1770 |
| 1986 | 2033 | 436 | 2469 |
| 1987 | 2600 | 595 | 3195 |
| 1988 | 3137 | 732 | 3869 |
| 1989 | 2641 | 726 | 3367 |
| 1990 | 1962 | 580 | 2542 |
| 1991 | 693 | 267 | 960 |
| 1992 | 434 | 184 | 618 |
| 1993 | 735 | 267 | 1002 |
| 1994 | 477 | 118 | 595 |
| 1995 | 265 | 103 | 368 |
| 1996 | 288 | 96 | 384 |
| 1997 | 259 | 167 | 426 |
| 1998 | 180 | 100 | 280 |
| 1999 | 143 | 61 | 204 |
| 2000 | 120 | 46 | 166 |
| 2001 | 96 | 36 | 132 |
| 2002 | 79 | 43 | 122 |
| 2003 | 162 | 72 | 234 |
| TOTAL | 65811 | 13822 | 67633 |

**Chanzo: Taarifa za NCI**

Mpango wa Elimu Huria na Masafa ni sehemu ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Sekondari (MMES) kama njia mbadala ya kuongeza idadi ya wahitimu na kuboresha elimu ya sekondari nchini. Mpango wa MMES ulikuwa wa miaka mitano (2004 -2009) ukiwa na lengo la kuandikisha walengwa 50,000 kupitia mfumo wa elimu usio rasmi. Mpaka kufikia mwezi Machi 2009 TEWW imeweza kusajili wanafunzi 39,686 kati yao wanaume ni

18,336 na wanawake 21,350 hivyo kufikia takriban asilimia sabini na tisa (79.4%) ya lengo la kitaifa kama inavyoonyeshwa katika jedwali Namba 7.

## Jedwali Na 7: Udahili wa Wanafunzi wa Masomo ya Elimu Huria na Masafa, Tanzania Bara: 2004 - 2011

| MKOA | 2004 | | | 2005 | | | 2006 | | | 2007 | | | 2008 | | | 2009 | | | Jumla Kuu | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | M | K | J | M | K | J | M | K | J | M | K | J | M | K | J | M | K | J | M | J | K |
| Arusha | 40 | 93 | 133 | 199 | 299 | 498 | 157 | 297 | 454 | 175 | 161 | 336 | 230 | 349 | 579 | 152 | 180 | 332 | 953 | 1379 | 2332 |
| Kagera | 0 | 0 | 0 | 31 | 22 | 55 | 111 | 138 | 249 | 112 | 131 | 243 | 189 | 201 | 390 | 152 | 122 | 274 | 597 | 614 | 1211 |
| Dar | 1165 | 1435 | 2600 | 768 | 930 | 1698 | 739 | 962 | 1701 | 466 | 693 | 1159 | 198 | 236 | 434 | 83 | 84 | 167 | 3419 | 4340 | 7759 |
| Dodoma | 72 | 64 | 136 | 122 | 204 | 326 | 128 | 235 | 363 | 143 | 168 | 311 | 120 | 246 | 366 | 100 | 167 | 267 | 685 | 1084 | 1769 |
| Iringa | 28 | 56 | 84 | 34 | 45 | 79 | 49 | 85 | 134 | 193 | 313 | 506 | 93 | 201 | 294 | 202 | 234 | 436 | 599 | 934 | 1533 |
| Pwani | 23 | 37 | 60 | 7 | 23 | 30 | 81 | 118 | 199 | 96 | 171 | 267 | 71 | 103 | 174 | 67 | 101 | 168 | 345 | 553 | 898 |
| Kigoma | 9 | 26 | 35 | 80 | 109 | 189 | 0 | 0 | 0 | 39 | 7 | 46 | 21 | 7 | 28 | 9 | 5 | 14 | 158 | 154 | 312 |
| Lindi | 22 | 29 | 51 | 39 | 64 | 103 | 19 | 47 | 66 | 21 | 29 | 50 | 33 | 21 | 54 | 8 | 54 | 62 | 142 | 244 | 386 |
| Mara | 268 | 202 | 470 | 520 | 489 | 1009 | 377 | 436 | 813 | 280 | 301 | 581 | 185 | 198 | 383 | 66 | 92 | 158 | 1696 | 1718 | 3414 |
| Manyara | 6 | 32 | 38 | 86 | 93 | 179 | 79 | 91 | 170 | 37 | 40 | 77 | 57 | 76 | 1133 | 29 | 48 | 77 | 294 | 380 | 674 |
| Mbeya | 30 | 25 | 55 | 50 | 40 | 90 | 47 | 23 | 70 | 67 | 45 | 112 | 75 | 67 | 142 | 63 | 117 | 180 | 332 | 317 | 649 |
| Morogoro | 26 | 53 | 79 | 163 | 155 | 318 | 151 | 79 | 230 | 32 | 71 | 103 | 55 | 80 | 135 | 102 | 99 | 201 | 529 | 537 | 1066 |
| Mtwara | 23 | 14 | 37 | 25 | 34 | 59 | 19 | 16 | 35 | 39 | 30 | 69 | 94 | 67 | 161 | 58 | 66 | 124 | 258 | 227 | 485 |
| Mwanza | 145 | 102 | 247 | 212 | 64 | 276 | 750 | 569 | 1319 | 341 | 203 | 544 | 277 | 245 | 522 | 169 | 301 | 470 | 1894 | 1484 | 3378 |
| K'njaro | 14 | 11 | 25 | 6 | 11 | 17 | 87 | 153 | 240 | 141 | 238 | 379 | 137 | 220 | 357 | 157 | 246 | 403 | 542 | 879 | 1421 |
| Rukwa | 70 | 85 | 155 | 62 | 90 | 152 | 65 | 67 | 132 | 220 | 180 | 400 | 120 | 110 | 230 | 45 | 39 | 84 | 582 | 571 | 1153 |
| Ruvuma | 251 | 304 | 555 | 210 | 205 | 415 | 168 | 230 | 398 | 151 | 258 | 409 | 224 | 283 | 507 | 201 | 229 | 430 | 1205 | 1509 | 2714 |
| S'nyanga | 151 | 136 | 287 | 141 | 100 | 241 | 504 | 194 | 698 | 208 | 146 | 354 | 299 | 464 | 763 | 565 | 594 | 1159 | 1868 | 1634 | 3502 |
| Singida | 87 | 114 | 201 | 87 | 105 | 192 | 86 | 91 | 177 | 104 | 70 | 174 | 140 | 134 | 274 | 132 | 104 | 236 | 636 | 618 | 1254 |
| Tabora | 182 | 255 | 437 | 343 | 342 | 685 | 310 | 529 | 627 | 221 | 266 | 487 | 106 | 46 | 252 | 85 | 75 | 160 | 1247 | 1613 | 2860 |
| Tanga | 23 | 59 | 82 | 53 | 118 | 171 | 98 | 124 | 222 | 53 | 55 | 108 | 46 | 60 | 106 | 82 | 145 | 227 | 355 | 561 | 916 |
| Jumla | 2635 | 3132 | 5767 | 3240 | 3542 | 6782 | 4025 | 4484 | 8509 | 3139 | 3576 | 6715 | 2770 | 3514 | 6284 | 2522 | 3102 | 5629 | 18336 | 21350 | 39686 |

**Chanzo: Taarifa za Idara ya Elimu Masafa**

### 3.3.3 Kufanya Utafiti wa Awali

Mnamo mwaka 2005 TEWW ilifanya utafiti kuhusu hali ya Elimu Masafa katika Tanzania. Utafiti huu ulihusisha mikoa yote 21 ya Tanzania Bara, wilaya mbili kila mkoa (3 kwa Dar es Salaam) na kata moja kila wilaya; jumla kata 43. Walioshiriki kujibu madodoso katika utafiti huo ni maafisa elimu wa mikoa na wilaya, waratibu wa elimu wa kata, walimu wakuu na wahitimu wa shule za msingi. Madodoso hayo yalikusanya takwimu kuhusu wahitimu wa shule za msingi, idadi ya taassisi za elimu, upatikanaji wa walimu, mahali pa kujifunzia na watoto wenye mahitaji maalum. Hojaji zilikusanya maoni toka kwa wazazi, wanajamii, taasisi zisizo za kiserikali na za kijamii, walengwa wenyewe. Ili kuhakiki taarifa na takwimu zilizokusanywa kwa madodoso, watafiti walitembelea sehemu husika. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuhitajika kwa masomo ya elimu ya sekondari kupitia njia ya Elimu Huria na Masafa, na utayari wa jamii na utashi wa serikali kuuunga mkono.

### 3.3.4 Kuandaa Mtaala

Mwaka 2004, TEWW iliweza kuandaa mtaala ambao, pia, unaonesha viashiria vinavyotumika kupima mafanikio ya walengwa. Mtaala huu umeandikwa kwa ustadi kiasi cha kumwezesha mlengwa kumaliza masomo ya sekondari kwa kuanzia miaka miwili badala ya minne, kwa kujumuisha usomaji wa moduli na masomo ya ana kwa ana.

### 3.3.5 Kuandaa Mihtasari

TEWW imekwisha andaa mihtasari ya masomo saba (Biolojia, Hisabati, Kiswahili, Historia, Uraia, Kingereza na Jiografia) kwa ajili ya mafunzo kwa njia ya Elimu Huria na Masafa. Mihtasari hii ni ya pekee kwa kuwa, pamoja na mambo mengine, imezingatia pia walengwa wenye mahitaji maalum (wenye ulemavu tofauti tofauti).

### 3.3.6 Utoaji wa Mafunzo Maalumu

TEWW imetoa mafunzo maalumu kwa walimu wa sekondari na waandishi wa mihtasari iliyotajwa juu. Mafunzo hayo yalilenga kujenga uwezo wa jinsi ya kuandika katika mtindo wa moduli badala ya vitabu vya kiada vinavyotumika katika shule za sekondari za kawaida, na jinsi ya kufundisha kwa njia ya elimu huria na masafa na kujifunza kwa ufanisi kwa kutumia moduli na kuhudhuria vipindi vichache vya ana kwa ana.

### 3.3.7 Moduli Zilizoandikwa na Nakala zilizochapishwa

Moduli za masomo saba ya elimu ya sekondari ziliandikwa kwa ajili ya hatua mbili zifuatazo:

- Hatua ya kwanza, sawa na kidato cha I na II: nakala 164,000; na
- Hatua ya pili, sawa na kidato cha III na IV: nakala 114,000.

Jumla ya moduli zilizoandikwa ni 278,000. Moduli zote zilisambazwa katika vituo 21 Tanzania Bara. Moduli hizo zinatumiwa pia na wanafunzi wa shule za sekondari, ili kukabili tatizo la uhaba wa vitabu na walimu shuleni.

### 3.3.8 Kuandaa Miongozo

TEWW imeandaa miongozo saba (7) inayowasaidia walengwa kujisomea na kufanya kwa makini mazoezi yaliyomo kwenye moduli zao. Pia miongozo inatoa maelekezo ya ufanisi kwa watendaji wakiwemo wawezeshaji, waratibu wa vituo na wakufunzi wakazi wa mikoa. Aidha, imeandaliwa miongozo maalum kwa ajili ya uandaaji na utoaji mafunzo yanayojenga uwezo kwa timu ya wawezeshaji kitaifa, wawezeshaji na waratibu vituoni pamoja na uhamasishaji ngazi za kata, wilaya na taifa.

### 3.3.9 Kuandaa na Kuendesha Mafunzo kwa Waratibu na Walimu wa Vituo vya Elimu Masafa

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeweza kutoa mafunzo kwa waratibu na walimu wa vituo vya elimu masafa wapatao 300 kati ya 1,151 waliobainishwa wakati wa zoezi lililofanyika mwaka 2004/2005 katika mikoa minne kwa kuanzia. Walimu hao tayari wamepitia mafunzo vyuoni na wana uzoefu wa kufundisha katika mfumo rasmi wa elimu

### 3.3.10 Uhamasishaji wa Viongozi na Watendaji Ngazi ya Mkoa na Wilaya

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, imefanya uhamasishaji wa jumla juu ya Elimu Masafa kitaifa kupitia nyombo vya habari kama redio, luninga, magazeti, mikutano ya hadhara na kamati za maendeleo (RCC) katika baadhi ya mikoa pamoja na kutawanya vijarida (information booklets) kila kata Tanzania Bara. Viongozi wapatao 273 wameshiriki katika warsha na kutoa mapendekezo ya utekelezaji wa programu ya elimu masafa ndani ya mikoa yao.

### 3.3.11 Maandalizi ya Rasimu ya Sera Shirikishi (Partnership Policy) ya Elimu Masafa

TEWW ilifanya maandalizi ya rasimu ya Sera Shirikishi ya Elimu Masafa yaliyohusisha wataalamu kutoka makao makuu ya Wizara ya Elimu, Baraza la Mitihani Tanzania na wadau wengine. Sera inalenga kutoa maelekezo makini kwa wadau wote wanaotoa elimu kupitia mfumo usio rasmi ili waweze kutoa elimu bora inayokidhi mahitaji ya taifa na kimataifa. Aidha sera hiyo inalenga kuboresha utoaji elimu nje ya shule na kuzuia mtindo uliozuka miongoni mwa jamii kutoa elimu hiyo holela, pasipo kuzingatia kanuni na sheria.

Pia, sera hii itaisaidia serikali na Baraza la Mitihani la Taifa (National Examination Council of Tanzania - NECTA) kutoa maelekezo kwa urahisi juu ya watahiniwa wote wa kujitegemea (Private candidates) na udhibiti wa usajili wa watahiniwa hawa kufanywa chini ya usimamizi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kupitia vituo vyote ishirini na moja (21) vya mikoa ya Tanzania Bara. Aidha, hatua hii itasaidia kudhibiti utoaji wa vyeti, udhibiti wa mitihani na kuweza kutoa wahitimu wenye kiwango bora cha elimu katika mfumo wa elimu usio rasmi.

### 3.3.12 Mpango wa Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi

Huu ni mpango ulioanzishwa ili kukidhi haja ya upatatikanaji wa elimu nje ya mfumo rasmi. Awali, mpango ulilenga kuwapatia wahitimu Mpango wa Elimu ya Msingi kwa Walioikosa (MEMKWA) kundi rika la pili nafasi ya kujiendeleza hadi elimu ya sekondari. Utafiti uliofanywa na TEWW kwa

msaada wa UNICEF katika wilaya saba tarajali (Temeke, Bagamoyo, Hai, Siha, Makete, Mtwara (V) na Magu) ulibainisha mahitaji ya kielimu ya walengwa; na kwamba kulikuwa na haja ya kuwa na mpango unaokidhi mahitaji ya wote waliokosa fursa ya elimu baada ya kumaliza elimu ya msingi. Hivyo, mpango huu unatekelezwa katika wilaya zote tarajali zilizotajwa awali. Malengo ya mpango ni kama yafuatayo:

i) Kutoa fursa ya elimu na ufundi stadi kwa makundi ya vijana na watu wazima walio pembezoni;

ii) Kupanua mawanda ya maarifa, stadi na misingi ya elimu waliyoipata katika ngazi ya msingi;

iii) Kuwaandaa walengwa kwa masomo ya ngazi za juu, ufundi na mafunzo ya kazi za utaalamu;

iv) Kuwawezesha walengwa kujitambua, kuwa raia makini, kushiriki katika shughuli za maendeleo, na kuwa wazalendo;

v) Kuwawezesha walengwa kufanya uamuzi sahihi juu ya fursa za kazi (carreer options) katika maisha;

vi) Kuwa na moyo wa kujiendeleza kielimu, kiuchumi na kimaisha kwa ujumla; and


vii) Kuandaa walengwa kwa elimu isiyo na mwisho wala mipaka.

Ili kutimiza malengo haya, mpango huu unajumuisha maeneo matatu ya kujifunza. Maeneo hayo ni taaluma, ufundi stadi na stadi nyenzo. Programu hii inatolewa kwa kutumia mfumo wa Elimu Masafa na Ana kwa Ana (Open and Distance Learning - ODL). Pia, inalenga kuboresha programu inayotolewa na TEWW ya masomo ya elimu ya sekondari (ODL) ambayo inatilia mkazo masomo ya taaluma pekee. Fursa ambayo, kufuatana na utafiti uliofanywa, walengwa waliona haikidhi mahitaji yao, hivyo, kuwepo umuhimu wa kuwa na programu jumuishi ya elimu changamani ambayo ina

taaluma, ujuzi na stadi za maisha. Mpango huu unatoa fursa ya kupata cheti cha ujuzi "Certificate of Competence" kwa muda mfupi.

Pia programu hii kwa kujumuisha taaluma, ujuzi na stadi za maisha, itatoa wahitimu watakaoweza kujiendeleza kitaaluma na katika fani ya ufundi baada ya kumaliza masomo yao. Vile vile itaboresha programu zinazotolewa na vyuo vya maendeleo kwa kutoa fursa ya kusoma masomo yanayojumuisha taaluma na kutambuliwa.

**Programu ya Elimu Changamani**




## 3.4 Uratibu wa Vituo Mikoani

Lengo kuu la kuanzishwa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ni kuelimisha wananchi katika maeneo yote ya mjini na vijijini. Kwa hiyo, TEWW ilianzisha ofisi zake kila mkoa wa Tanzania Bara ambazo zinawajibika na uratibu wa shughuli zote za TEWW huko mikoani. Vituo hivyo vilianzishwa kwa nyakati tofauti kufuatana na upanuzi wa shughuli za TEWW ulivyokuwa unaendelea mwaka hadi mwaka kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| 1963/64 | - | Dar es Salaam, Mbeya na Moshi |
| 1965 | - | Mwanza |
| 1972 | - | Songea |
| 1974 | - | Tabora |
| 1975 | - | Morogoro, Mtwara, Dodoma na Bukoba |
| 1976 | - | Musoma |

| | | |
|---|---|---|
| 1977 | - | Sumbawanga, Kigoma na Arusha |
| 1978 | - | Lindi, Tanga na Singida |
| 1979 | - | Kibaha, Iringa na Shinyanga |
| 2000 | - | Manyara. |

Uratibu wa vituo mikoani ulianzishwa kuratibu, kusimamia, kufuatilia, kuhakiki na kutoa miongozo ya utekelezaji wa shughuli za vituo ili kufanikisha na kuendeleza jamii kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

### 3.4.1 Shughuli mbalimbali ambazo hufanyika mikoani

Shughuli za vituo mikoani hutekelezwa na wafanyakazi wapatao sita mpaka kumi kwa kila kituo, ambao ni Mkufunzi Mkazi mmoja wa mkoa na wasaidizi wake, wakiwemo: Mhasibu, Katibu Muhtasi, Mhudumu, Dereva na Walinzi. Vituo hivyo husimamia shughuli muhimu za Taasisi zifuatazo:

i) Kuendesha na kuratibu masomo ya jioni; semina; warsha; mafunzo ya redio kwa vikundi; na sinema;

ii) Kufanya tafiti; kufuatilia, kukusanya na kutunza takwimu mbalimbali katika Nyanja za elimu ya watu wazima ili kuweza kupanga mipango endelevu katika kila mkoa;

iii) Kuendesha masomo ya sekondari kupitia elimu huria na masafa, ambapo shughuli za vituo zinajumuisha:

- Kuratibu shughuli zote za uendeshaji za ENP,
- Kuhamasisha wateja,
- Kuandikisha wanaojifunza,
- Kutafuta walimu,
- Kutafuta maeneo na kuanzisha madarasa,
- Kukusanya karo na malipo mengine yote,
- Kuratibu utekelezaji wa mpango wa elimu masafa na masomo ya ana kwa ana, na
- Kuwasiliana na makao makuu kwa taratibu zilizowekwa.

iv) Kuratibu mafunzo maalumu kwa walimu nje ya shule. Huu ulikuwa ni mradi wa Wizara ya Elimu ulioanzishwa 1975. Vituo vya TEWW vilikuwa vinakagua walimu na kuhakiki mitihani pamoja na kushiriki katika usahihishaji;

v) Kuendesha na Kuratibu Shule za mwisho wa wiki kwa ajili ya walengwa wanaojiandaa kufanya mitihani ya kujiunga na elimu ya juu kama watu wazima; na

vi) Kuendesha Miradi ya Mafunzo Ufundi, kwa mfano katika miaka ya 70 TEWW ilikuwa inatoa mafunzo kwa vikundi mbalimbali ambavyo vilikuwa vinaendesha miradi ya ujasiriamali kama ilivyoonyeshwa katika utekelezaji wa shughuli za Idara ya Elimu kwa Umma na Maendeleo ya Wanawake.

Mwaka 2007, 'Plan International' ilikabidhi mradi wake, wa kuendeleza vijana huko Mwanza kwa TEWW, baada ya kuona kuwa TEWW ina uwezo wa kuuendesha kutokana na uzoefu wake katika elimu nje ya mfumo rasmi. Mali zilizokabidhiwa ndani ya mradi huo zimesaidia kutoa mafunzo katika fani ambazo zinawezesha vijana kujiajiri. Fani hizo ni uashi, useremala, ushonaji, umakenika, kuunga vyuma na ufundi umeme. Baadhi ya mali zilizokabidhiwa ni:

- majengo ambayo ni pamoja na madarasa karakana na hostel mbili (2),
- vifaa vya uashi useremala, ufundi magari na ushonaji,
- pikipiki mbili aina ya Honda Trail 110, na
- mashine za kuranda na kusafisha mbao.

vii) Kuhamasisha na kuelimisha asasi mbali mbali kuhusu masuala mtambuka. Asasi nyingi zimeibuka, hasa, vijijini ambazo zinalenga kuelimisha jamii lakini hazijui mbinu za kuelimisha watu wazima. Kwa hiyo ni shughuli nyingine ambayo inafanywa na vituo kwa kushirikiana na wadau hao; na

viii) Kutoa Huduma za Maktaba kwa kufikisha huduma hizo kwa wananchi, kwa kushirikiana na wadau wengine ambao ni Wizara ya Elimu na

Maktaba Kuu ya Taifa. Lengo ni kuimarisha na kuendeleza maarifa na ujuzi wa walengwa kwa kuwawezesha kujisomea, kupata taarifa muhimu na endelevu ili waweze kwenda sambamba na mabadiliko ya mara kwa mara.

### 3.5 Utumishi, Utawala na Fedha

Shughuli za TEWW za utumishi na utawala zinahusisha usimamizi na maendeleo ya rasilimali watu, miundombinu na fedha kufuatana na sera na kanuni zilizopo ili kuleta tija. Aidha, baadhi ya shughuli mahsusi zilizotekelezwa katika eneo hili ni pamoja na:

i) Kuandaa na kuchapa mpango mkakati wa TEWW wa miaka mitano (5) kuanzia 2008/2009 - 2012/2013;

ii) Ufungaji wa mtandao wa kompyuta katika ofisi zote za makao makuu ya TEWW;

iii) Kukuza mtaji na kuongeza mali za shirika kwa kununua viwanja na majengo mapya vituoni pamoja na kupata hati za majengo na viwanja katika mikoa (11) ikiwemo Mbeya, Iringa, Lindi, Kilimanjaro, Manyara, Rukwa, Mwanza, Ruvuma, Morogoro na Dodoma;

iv) Kuboresha mazingira ya kazi kwa kukarabati na kujenga madarasa, kumbi za mikutano na mihadhara, maabara ya kompyuta, kuweka tovuti makao makuu, kuchimba kisima ili kupunguza tatizo sugu la maji, kununua vitendea kazi na kuboresha maktaba na kitengo cha uchapaji;

v) Kuongeza Idadi ya wataalamu katika fani mbalimbali na kuanzisha vitengo vipya ambavyo havikuwepo hapo awali, kitengo cha Tecknolojia ya Mawasiliano na Habari; Kitengo cha Ugavi; kitengo cha Ushauri Nasaha; Ofisi ya Mawasiliano na Masoko; na Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

vi) Kuongeza kasi ya kuendeleza wafanyakazi kitaaluma hasa baada ya TEWW kupata ithibati ya kutoa shahada ambayo inahitaji wataalam wengi wenye sifa ya ngazi ya shahada ya uzamili na uzamivu. Katika kipindi cha 1995-2005 na 2006-2011 idadi ya watumishi walioajiriwa na sifa zao zilikuwa kama inavyooneshwa katika jedwali namba 8.

**Jedwali Na 8: Idadi ya Watumishi na Sifa za Taaluma**

| Miaka | Sifa | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | PhD | MA, MBA, MSC | BA/BSC | Diploma | Jumla |
| 1995-2005 | - | 32 | 36 | 14 | 82 |
| 2006-2011 | 2 | 50 | 48 | 24 | 125 |

**Chanzo: Taarifa za Utumishi, TEWW**

vii) Kurekebisha na kuandaa miongozo ya utumishi ikiwemo: "Staff Regulations"; "Training and Development Policy"; "Scheme of Service" na "Accounting Manual"; Sheria ya Fedha; Sheria ya Ununuzi; " Audit Manual"; na Miongozo ya Ukaguzi wa Mahesabu ili kuhakikisha shirika linaendeshwa kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu;

viii) Kuimarisha mahusiano na ushirikiano na Taasisi mbalimbali za kitaifa na kimataifa kwa kushiriki makongamano, maonyesho na semina mbalimbali;

ix) Kuimarisha usafiri. Kwa mfano, katika kipindi cha kuanzia 2004 – 2009, TEWW iliweza kununua magari 12 ili kuboresha huduma za usafiri katika shughuli za shirika. Kabla ya hapo, magari ya TEWW yalikuwa yakipatikana kwa misaada ya wafadhili kama vile SIDA, UNICEF, Wizara ya Elimu na TACAIDS; na

x) Kuboresha huduma na maslahi ya wafanyakazi. Kwa mfano, kwa kushirikiana na chama cha wafanyakazi(RAAWU),TEWW imeweza kuwapatia wafanyakazi wa TEWW, makao makuu, viwanja 145 mjini Kibaha kwa ajili ya ujenzi wa makazi ya watumishi wa makao makuu na mkoa wa Pwani. Vilevile, imeanza kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wafanyakazi kwa ajili ya kuendeleza maisha yao; kuboresha msaada wa gharama za msiba na mazishi kwa wafanyakazi wanapofiwa au kufariki; na kuendeleza ofisi za kufanyia kazi kimandhari na vitendea kazi.

# SURA YA NNE

## 4.0 MAFANIKIO YA TEWW KATIKA KIPINDI CHA MIAKA 50 ILIYOPITA

Yapo mafanikio mengi ya TEWW yanayohusiana na mchango wake katika elimu na maendeleo ya taifa kwa ujumla. Baadhi ya mafanikio makubwa ni pamoja na:

i) kuwa sehemu muhimu ya sifa kubwa ambayo Tanzania ilipata katika miaka ya 1970 mpaka 1980 ambapo Tanzania iliweza kufikia asilimia 96 ya watu wanaoweza kusoma, kuandika na kuhesabu. Mwaka 1992, TEWW ilizawadiwa nishani na shirika la Kimataifa la UNESCO kwa kufanikisha kampeni ya kufuta ujinga Tanzania;

ii) kutoa jumla ya wahitimu 2,677 wa Stashahada ya Elimu ya Watu Wazima na 418 wa Stashahada ya Juu ya Elimu ya Watu Wazima kuanzia 1969 hadi 2011 kuanzia 1969 mpaka 2011;

iii) TEWW kupata ithibati ya NACTE, mwaka 2009 ambayo inawezesha TEWW kutoa mafunzo ya elimu ya juu na wahitimu wa programu zake za Astashahada, Stashahada na Shahada kutambulika kitaifa na kimataifa. Hii inawapa uwezo wa kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi, hasa kwa vile mitaala inayofundishwa inazingatia mahitaji halisi ya soko la ajira na umahiri katika kazi;

iv) kusogeza huduma kwa wananchi wengi zaidi nchini kutokana na kugatua usimamizi na uendeshaji wa shughuli za elimu masafa toka makao makuu kwenda mikoani. Elimu masafa kuchangia katika kufanikisha malengo ya elimu kwa wote na ya millennia nchini;

v) kuanzisha mpango wa elimu changamani ili kusaidia kuongeza upatatikanaji wa elimu nje ya mfumo rasmi inayounganisha masomo ya taaluma na ya ufundi stadi pamoja na stadi nyenzo (generic skills) ili kuwawesha wahitimu kujiajiri wenyewe; kuwa na uelewa mpana kimaisha; pia kupata fursa ya mafunzo ya juu zaidi kitaaluma na/au kiufundi. Hii itapunguza idadi ya vijana wanaokosa fursa za kujiendeleza kielimu na ajira;

vi) kuendesha kampeni zaidi ya kumi na mbili (12) kuanzia 1969 - 2011, kama zilivyochanganuliwa katika sura ya tatu, ambazo zilisaidia wananchi kupata elimu ya masuala mtambuka;

vii) kutoa machapisho mabali mbali kwa ajili ya kuelimisha umma, kwa mfano vitabu (Taz. Kiambatisho); majarida: "Journal of Adult Education" – Namba 1 mpaka 18, "Studies in Adult Education"– Namba 1 mpaka 66; Sauti ya Wanawake – Namba 1 mpaka 5;

viii) kuanzisha studio ya kisasa ya kuelimisha umma juu ya masuala mbalimbali ili walengwa waweze kujiendeleza na kushiriki katika mipango ya maendeleo ya nchi;

ix) kuanzisha huduma za ushauri nasaha kwa wafanyakazi na wanafunzi na wanaoishi na VVU na wasiokuwa navyo kuzuia maambukizi, kuzuia unyanyapaa na kuwezesha waathirika kuishi kwa matumaini.

x) kuteuliwa kuratibu na kuendesha mafunzo ya mbinu za kufundisha mtaala unaozingatia umahiri na mahitaji ya soko la ajira na kazi katika vyuo vyote vya elimu ya juu vinavyosimamiwa na NACTE nchini. Imetoa mafunzo haya kwa vyuo vifuatavyo:
- Chuo cha Polisi (CCP) - Moshi,
- Chuo cha Uhamiaji – Moshi,
- Institute of Accountancy Arusha,
- Waadishi wa habari toka vyuo vya Uandishi wa Habari,
- Chuo cha Polisi Zanzibar,
- Mweka Wildlife Institute,
- Chuo cha Polisi Kurasini, Dar es Salaam,
- Tanzania Institute of Accountancy - Dar es Salaam,
- Mwlimu Nyerere Memorial Accademy (MNMA), na
- Institute of Tax Management, Mikocheni – Dar es Salaam.

xi) kutoa elimu ya kijiendeleza kwa walengwa wengi, miongoni mwao wamo waliowahi kuwa viongozi wa ngazi za juu serikalini kama vile: Hayati

Rashidi Mfaume Kawawa (Waziri Mkuu, Makamu wa Kwanza wa Rais); Hayati Adam Sapi Mkwawa (aliyewahi kuwa Spika wa Bunge la Muungano); Mheshimiwa Simon E. Chiwanga(aliyewahi kuwa Waziri wa Elimu); Mheshimiwa Joseph Kabila (Rais wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo).

xii) Kuanzisha programu ya Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Endelezi (Adult and Continuing Education) ili kuchangia ongezeko la walio na elimu ya juu nchini. Tangu ilipoanza mwaka 2009/2010 hadi 2010/2011, jumla ya wanafunzi 238 walisajiliwa.

xii) Kushirikiana na Taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi katika kutekeleza majukumu yake. Ushirikiano huu umeleta mafanikio kwa Taasisi na taifa kama ifuatavyo:

- **Benki ya Dunia**, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, (kuendesha mradi wa elimu ya sekondari kupitia Mpango wa elimu masafa, ambapo Walengwa 39,000 wamenufaika),
- **Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania na, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Kutengeneza mtaala wa elimu** masafa; kutoa mafunzo kwa wawezeshaji ili waweze kutumia mtaala huu kutengeneza moduli, mihutasari na miongozo mbalimbali ya Elimu Masafa; na kuendesha mafunzo ya kuwajengea uwezo wawezeshaji ),
- **German Adult Education Association (DVV)** (Ufadhili wa mafunzo ngazi ya cheti na stashahada kwa wataalam wa elimu ya watu wazima), kwa miaka 12. Wataalam hao wengi wanaendeleza elimu ya watu wazima huko wilayani kote nchini. Pia shirika hili linasaidia kuchapa majarida ya JAET na SAED na vitabu vingine vingi kwa kipindi hicho chote,
- **UNICEF** (Programu ya Elimu Changamani Baada ya Elimu ya Msingi, kwa Kingereza, 'Integrated Post Primary Education'(IPPE) iliyoyoanza mwaka 2006), pia kutoa mafunzo kwa waratibu wa MEMKWA ngazi ya wilaya na kata pamoja na walimu wakuu wa

shule za msingi zenye vituo hivyo na kuandika vitabu vya Mama na mtoto, Haki za mtoto, Haki za wanawake na Athari za ukeketaji),

- **Chuo Kikuu cha Kyambogo, Uganda** (kutoa Mafunzo ya Uratibu na Usimamizi wa Elimu Masafa, kwa msaada wa COL),
- **Commonwealth of Learning (COL)** (Ufadhili wa mafunzo yahusuyo Elimu Masafa kwa wahadhilri na wakufunzi),
- **TACAIDS** (Mafunzo ya jinsi ya kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI na utoaji huduma kwa wafanyakazi wanaoishi na virusi vya UKIMWI pamoja na jamii kwa ujumla), na
- **UNESCO** (Kuandika vitabu vinavyozingatia jinsia na mahitaji ya walengwa, 1. vya kujifunzia kusoma, kuandika na kuhesabu: Usawa na Maisha Bora ya Familia, Kiongozi chake; na 2. cha kujiendeleza: Elimu ya Miradi ya Kiuchumi).

xiv) Kuandaa mtaala na muhtasari na kuendesha mafunzo ya wawezeshaji 4000 wa wakimbizi wa Afrika ya Kusini walioishi Tanzania, Zambia na Uganda katika masomo ya Kingereza, Hisabati na Kilimo ambao baada ya nchi zao kupata uhuru, waliweza kushiriki katika kujenga nchi hizo.

xv) Kununua majengo katika mikoa ya Rukwa, Dodoma, Kilimanjaro, Ruvuma; kununua viwanja Rukwa, Manyara, Mwanza, Tanga, Dar es Salaam; kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano (5) (2008/2013); na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na kufundishia makao makuu na mikoani.

# SURA YA TANO

## 5.0 CHANGAMOTO ZILIZOIKABILI TEWW MIAKA 50 ILIYOPITA

Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kipindi cha miaka 50, TEWW ina changamoto kadhaa kama ifuatavyo:

i) kupungua umaarufu wa TEWW kama mdau muhimu katika kuhamasisha jamii kuleta maendeleo ya nchi;

ii) kuendelea kupungua kwa ruzuku, hivyo, kuifanya TEWW ishindwe kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi;

iii) kukosekana kwa miundo mbinu na vitendea kazi vya kisasa vya kutosha, kama vile majengo na TEHAMA;

iv) kukosekana sera ya kitaifa ya utoaji wa elimu ya watu wazima na elimu masafa ambayo inaongoza utoaji wa elimu hiyo nchini;

v) jamii kutotambua umuhimu wa elimu masafa na endelevu katika kuleta maendeleo ya mtu binafsi na taifa kwa ujumla;

vi) kutokuwepo uwiano stahiki wa mgawanyo wa raslimali fedha kati ya mfumo rasmi na usio rasmi;

vii) kutokuwa na wataalamu wa kutosha waliobobea katika elimu ya watu wazima na mfumo usio rasmi;

viii) kutokuwa na vyombo vya kutosha vya usafiri kwa ajili ya kufuatilia na kuratibu uendeshaji wa elimu masafa na programu nyingine mikoani;

ix) kushindwa kupanua ushirikiano wa TEWW na vyuo vingine nje ya Tanzania, Afrika Mashariki na SADC;

x) kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya mafunzo ya muda mfupi hasa yanapohitajika kwa haraka kama vile wakati wa maafa; na

xi) kutokidhi mahitaji kwa sheria inayounda TEWW, kimuundo na kimajukumu, kwa maana ya kuwa na vyuo vya elimu ya juu vinavyojitegemea chini ya Mkurugenzi Mkuu vikiongozwa na wakuu wa vyuo (Principals).

# SURA YA SITA

## 6.0 MATARAJIO YA TEWW KATIKA MIAKA 50 IJAYO

Kauli mbiu ya TEWW itaendelea kuwa "Elimu Haina Mwisho".Katika miaka 50 TEWW ijayo, inalenga kuwa taasisi inayoongoza katika kutoa mafunzo na Elimu ya Watu Wazima (EWW) katika mfumo usio rasmi, yenye ubora wa hali ya juu na kuwa na wataalam mahiri katika tafiti, kubuni, kuandaa na kuendesha programu changamani za EWW na maendeleo ya jamii ambazo ni endelevu na kwa rika zote. Majukumu makuu ya TEWW yataendelea kuwa: kutoa mafunzo na elimu kwa wataalam wa EWW na elimu katika mfumo usio rasmi; kudumisha na kuendeleza utoaji wa elimu kwa ujifunzaji Huria na Masafa, kutafiti na kutoa machapisho ya elimu kwa umma na EWW; kushauri na kujenga ushirikiano na wadau wengine wa EWW na ya kujiendeleza ndani na nje ya nchi.

Hivyo, kwa miaka 50 ijayo, TEWW inatarajia kufanya yafuatayo:

a) Kupanua utoaji wa programu za mafunzo ya wataalamu wa Elimu ya Watu Wazima, Maendeleo ya Jamii na Elimu kwa Umma:

   i. Kuanzisha na kuimarisha matawi ya programu endelevu na zinazozingatia soko la ajira na utendaji mahiri katika mikoa yote Tanzania bara na Visiwani, ili kutoa elimu na mafunzo kwa walengwa wengi zaidi hasa vijijini, watakaoweza kushiriki kikamilifu katika kuleta maendeleo ya taifa, kudumisha utawala bora, kupambana na adui ujinga, maradhi na umasikini.

   ii. Kushirikiana na vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kutoa wataalam waliobobea katika masuala ya EWW, Elimu huria na masafa wenye uwezo wa kuandaa mitaala changamani, kufanya utafiti, kuandika vitabu na kuendesha programu za elimu watu wazima na na endelezi.

   iii. Kuwa na maktaba za kisasa ambazo zitakuwa kisima cha maarifa na ujuzi cha EWW na mfumo usio rasmi zenye vitabu vya kutosha kwa kila mlengwa, machapisho na matumizi makubwa ya teknolojia/TEKNOHAMA. Pia kuwa na matawi katika kata zote za

Tanzania yenye kudumisha tabia ya kupenda kusoma wakati wote, hivyo kufuta ujinga ambao ni adui mkubwa wa maendeleo.

iv. Kupata eneo mkoa wa Pwani ili kujenga makao makuu ya TEWW yenye ofisi za kutosha, kumbi za mikutano za kisasa, madarasa, hosteli, nyumba za wafanyakazi, maabara za kompyuta na kufundishia lugha za kigeni. Sehemu za burudani kwa huduma muhimu (benki, zahanati), bwawa la kuongelea, viwanja vya michezo na bustani ya kumpumzika.

b) Kuimarisha na kupanua utoaji wa programu za mafunzo na za elimu huria na masafa:

i. Kuifanya idara ya Elimu kwa Njia ya Posta (ENP) kwa sasa Idara ya Elimu Masafa iliyoanzishwa kama "National Correspondence Institute (NCI)" 1972 yenye sub-vote: 270324 chini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuwa Chuo cha Kitaifa cha Elimu Masafa Tanzania "Tanzania College of Open and Distance Learning (TACODL)". Taasisi hiyo itasimamia utoaji elimu huria na masafa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari na elimu isiyo ya chuo kikuu ili kutoa fursa kwa wanaoikosa kwa sababu mbalimbali.

ii. Kuwa na mtandao wa vituo vya kutoa elimu kwa njia ya Elimu Huria na Masafa katika mikoa na wilaya zote Tanzania Bara na Visiwani vyenye uwezo wa kutoa elimu na mafunzo yanayozingatia stadi za kazi, maarifa na mahitaji ya soko la ajira ili kuwa na wahitimu mahiri wenye uwezo wa kutumia fursa zilizopo, kujiajiri na kuleta maendeleo endelevu kwao binafsi na taifa kwa ujumla.

iii. Kuanzisha programu za Astashahada, Stashahada na Shahada zinazoendana na mahitaji ya kupanuka kwa wigo wa Elimu ya Watu Wazima na kujifunza kusiko na kikomo kwa njia ya elimu huria na masafa ili kuwafikia walengwa wengi zaidi;

iv. Kutekeleza sera ya kitaifa ya Elimu Huria na Masafa ambayo inaandaliwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya nchi za kusini mwa Africa (SADC) pamoja na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na Chuo kikuu Huria.

v. Kusimamia na kuendeleza utoaji wa Elimu Changamani baada ya Elimu ya Msingi (Integrated Post Primary Education - IPPE) nchini Tanzania inayojumuisha taaluma, stadi za kazi na maarifa ya lugha pamoja na uraia na haiba njema. Pia kuwa na vituo vya kujiendeleza kielimu kwa asilimia 85 ya wahitaji wote nchini ambavyo vitaendeshwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama itakavyofafanuliwa na mkakati wa sera ya Elimu masafa.

vi. Kufanya tafiti ili kuchangia maarifa katika eneo la Elimu ya Watu Wazima na elimu huria na masafa.

c) Kuimarisha na kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa:

i. kupitia kampeni za kitaifa, warsha na mafunzo ya muda mfupi na makongamano yanayohusu masuala ya maendeleo kama vile utunzaji wa mazingira, jinsia, haki za binadamu, uchumi endelevu, afya na usafi wa mwili.

ii. kuelimisha umma juu ya kilimo bora na lishe bora, kwa kutumia TEHAMA, Redio, Televisheni na magari ya matangazo yenye kuwafikia wananchi wengi ili kuwa jamii iliyoelimika, yenye uelewa mpana na inayotambua wajibu wake katika taifa.

iii. kupanua na kuboresha shughuli za studio ya TEWW ili iweze kutayarisha na kurusha matangazo ya programu mbalimbali za kuelimisha jamii mijini na vijijini.

d) Kuanzisha kituo maalumu cha taifa na machapisho (documentation centre) ya Elimu ya Watu Wazima na maendeleo ya jamii chenye kutumia TEHAMA ya kisasa ili kutoa mawasiliano na taarifa kwa walengwa na wadau wengine.

## 0 HITIMISHO

iaka 50 ya Uhuru wa Tanzania Bara, imeshuhudia mafanikio makubwa atika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kama ilivyobainishwa ndani ya tabu hiki. Huduma za TEWW zimekuwa zikibadilika kulingana na mahitaji a watanzania na dunia kwa ujumla. Msingi mkubwa wa shughuli za TEWW mekuwa ni falsafa na mwelekeo wa wananchi, ambavyo vinatekelezwa upitia dira na dhima ya Taasisi.

atika kipindi chote cha miaka 50 TEWW imekuwa chachu kubwa ya aendeleo ya nchi kwa kutoa elimu kwa watu wazima kwa kada mbalimbali wa kutumia mbinu na njia zenye kuleta ufanisi kama vile elimu masafa, ampeni na mafunzo ya ana kwa ana.

amoja na mafanikio makubwa ya TEWW, zimekuwepo changamoto kama ile kiasi kidogo cha ruzuku kutoka serikalini, uhaba wa miundo mbinu ya ehama na matumizi yake hafifu katika utoaji wa Elimu ya Watu Wazima, punguful wa rasilimali watu na vitendea kazi. Hata hivyo, TEWW mejipanga vyema kukabiliana na changamoto zilizopo kupitia mpango nkakati wa kutekeleza majukumu yake unaolenga kutoa mchango mkubwa atika kuendeleza nchi kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia katika niaka 50 ijayo.

(TUMETHUBUTU, TUMEWEZA NA

TUNAZIDI KUSONGA MBELE)

**DESEMBA, 2011**

Imetayarishwa na:
TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA

S.L.P 20679, DAR ES SALAAM
SIMU: +225 22 2150836
NUKUSHI: +255 22 2150838
BARUA PEPE: info@iae.ac.tz
TOVUTI: www.iae.ac.tz